# *Njia Ya Kurudi*

Mwaweza kuketi. [Unabii unatolewa. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Inapendeza sana kuona urahisi wa utendaji kazi wa Roho na watu ambao ni wanyenyekevu vya kutosha kulisikiliza na kuliamini, na kulishika tu, jinsi tunavyoshukuru, hilo himizo kutoka kwa Mungu kwamba tunapaswa kuwa tunangojea, na Yeye atafanya kazi kati yetu, tunamshukuru.

2 Sasa, nilichukua muda mrefu kidogo jana usiku, nimeingia tu na, dakika chache zilizopita, na—nami nilisikitika, kuwaweka mmesimama namna hiyo, nami ninajaribu kuharakisha usiku wa leo, kama nikiweza. Na kesho asubuhi, kifungua kinywa cha Wafanyabiashara huko Washington-Youree, nami ndio kwanza niambiwe na ndugu mmoja, ambaye ana tiketi, kwamba tiketi zinapaswa kununuliwa usiku wa leo, kwa ajili ya kupata nafasi ya kutosha, wapate kujua wakati watakapouza nafasi za kutosha asubuhi, wapate kuyaandaa mambo; naye akasema mhakikishe mmekata tiketi zenu, nami nadhani watakuwa mbele ya hicho chumba huko juu usiku wa leo.

3 Na kesho usiku, Bwana akipenda, nataka, sijui kamwe, bali nikifikiria tu kama Yeye akipenda, ningependa kuzungumza juu ya jambo moja maalum kesho usiku, hilo ni juu ya: *Tuna Vitu Vyote Katika Kristo*. Sasa, ni fungu dogo linalojulikana, lakini leo ndio kwanza linijie, nami nataka tu kulizungumzia kesho usiku, Bwana akipenda.

4 Na kisha nafikiri tuna Jumapili asubuhi, halafu Jumapili usiku, Bwana akipenda, ninataka kuhubiri juu ya somo: *Kuhesabu Kinyumenyume,* kujitayarisha kwa ajili ya kanisa kuondoka. Mnaona? *Kuhesabu Kinyumenyume*. Mnaona? Mnajua kuhesabu kinyumenyume ni nini. Na, ninaamini tunaweza kulithibitisha kwa Maandiko kwamba tuko sasa hivi katika kuhesabu kinyumenyume. Sasa, kwa hiyo mtuombee. Na, kama huna kanisa lolote unalohudhuria Jumapili asubuhi, tungefurahi kuwa nawe hapa, na Jumapili usiku, bila shaka, kama una kanisa lako mwenyewe hapo ndipo mahali pako pa kwanza pa wajibu, tunakutarajia uhudhurie hilo, lakini iwapo huna, mbona, tutafurahi kuwa nawe.

5 Nami nasikia kwamba usiku wa leo, endapo tunaweza kumaliza haraka vya kutosha, tutakuwa na m—mstari mdogo wa maombi. Billy alisema alisambaza kadi za maombi hapa, nafikiri hiyo ilikuwa ni kweli, naam, kwamba tutakuwa na mstari wa maombi kuwaombea wagonjwa.

6 Basi wakati mwingine mimi. . .Mtu fulani. . .Wengi wameniambia mara nyingi, kasema, "Unapaswa kubaki na

huko kuwaombea wagonjwa, hupaswi kujaribu kufanya hili lingine."

7 Lakini mtu fulani alinipigia simu si muda mrefu uliopita, kasema, "Kwa nini sikuzote unawakaripia hao wanawake?" Vema, siwakaripii. Akasema, "Vema," kasema, "kwa nini usiachane na hao wanawake?" Kasema, "Hao wanaume wote kuhusu madhehebu yao, na kila kitu . . . " ndugu mashuhuri sana.

Nami nikasema, "Huamini kwamba hilo ni la Kimaandiko kwao kufanya hivyo, sivyo?"

Akasema, "La." Lakini kasema, "Hivi Bwana hakukuita kuwaombea wagonjwa?"

Nikasema, "Naam."

Akasema, "Naam, kwa nini, usilizingatie hilo?"

Nikasema, "Nalizingatia."

Naye akasema, "Acha, kama Yeye alikuita kuwaombea wagonjwa, acha—acha—acha wahubiri washughulikie hilo."

Nikasema, "Lakini wao hawalishughulikii."

Akasema—akasema, "Mbona . . . "

Nikasema, "Si—sina budi . . . "

Akasema, "Mbona, watu wengi katika . . . Najua, nadhani, watu milioni moja wanakuchukulia kuwa nabii."

Nikasema, "Mimi si nabii."

Akasema, "Lakini watu wanakuwazia hivyo." Kasema, "Kusema ukweli, mimi nakuwazia hivyo."

8 Nikasema, "Asante." Nikasema, "Wakati mwingine Yeye ananionyesha mambo yanayokuja, wala hajawahi kunidanganya bado, wala hatanindanganya, maana Yeye ni Mungu, hawezi."

9 Kisha akasema, "Vema, kama wewe ni mtumishi wa Mungu namna hiyo, kwa nini usiwafundishe hao wanawake na kadhalika jinsi ya kupokea karama za juu za kiroho, badala ya kuendelea kuwagombeza juu ya kukata nywele zao, na kuvaa kaptura, na kujipodoa, na kadhalika?" Kasema, "Unapaswa kuwafundisha mambo makubwa zaidi, na jinsi wanavyoweza kupokea karama kuu, na kufanya jambo fulani."

10 Nikasema, "Utafundishaje aljebra wakati hata hawatasikiliza ABC zao? Wajifunze hizo, ndipo tutaanza na jambo lingine."

11 Kidogo linasikika la kukufuru, mhudumu mzee (Asante.), mhudumu mzee siku moja alikwenda kufanya m—mkutano mahali fulani, akasema—alihubiri usiku wa kwanza juu ya toba, usiku wa pili juu ya toba, usiku wa tatu, usiku wa nne, usiku wa tano. Mashemasi wakakutana naye huko nyuma na

kusema, "Ndugu, tunaufurahia ujumbe huo juu ya toba." Lakini wakasema, "Je, huna kitu kingine unachoweza kuhubiri?"

Akasema, "Loo, naam. Lakini hebu ngoja hata wote watubu kwanza, ndipo tutaanza jambo lingine."

12 Kwa hiyo, nikiingia katika nyumba ya Mungu na kuona kila kitu kimepangwa vizuri, basi tutaanza jambo lingine. Mnaona? Kwa hiyo—kwa hiyo tunaninii . . . Wewe . . . Ninatamani maombi yenu, sisemi mambo hayo nipate kuwa mbaya, mnajua hilo, ni—nina bidii. Ni binti za Mungu, ni wana wa Mungu, nasi tunapaswa kujiadabisha namna hiyo, tunapaswa kutenda hivyo na kujaribu kuja nalo. Nimepungukiwa sana nalo nami naomba mniombee, nami ninawaombea.

13 Kwa hiyo, tutaombeana, na labda siku moja Mungu atatuleta sote pamoja katika kitu *fulani* kikubwa kitakachotuondoa katika machafuko haya yote hapa kwa vyovyote vile. Kidogo ninachoshwa na maskini nyumba hii ya wadudu hata hivyo, nawe je? Ningependa kuchukua ndege ya peke yangu, moja ya asubuhi hizi, atakapokuja.

14 Sasa, nilitangaza jana usiku, kwamba baada ya kuzungumza juu ya yubile, na kutoa wito wa kurudi kwenye Pentekoste asilia, na kwenye Ujumbe, nilisema usiku wa leo nitajaribu kuzungumzia kidogo jinsi ya kurudi. Mnajua, hakuna haja ya kumwambia mtu yeyote la kufanya, isipokuwa uwaambie jinsi ya kulifanya. Jambo ndilo hilo.

15 Sasa, kuna—fungu la maneno ninalotaka kusoma, nime—nimelitumia hapo awali, lakini labda sio kwa njia hii hasa, lakini nilifikiri linaoana vizuri, nami sina budi tu kulileta kwa njia hiyo. Kwa hiyo, nafikiri kulileta hili juu ya jinsi ya kurudi, na ninii . . . kuna njia nyingi za kutoka, lakini kuna njia moja tu ya kurudi.

16 Nilikuwa . . . Jamaa mmoja alisema wakati mmoja huko—huko milimani, alikuwa . . . tulikuwa huko juu, mimi na jamaa mwingine, tuliokuwa waongozaji wenye leseni huko Colorado, alikuwa na kundi la watu ng'ambo ya pili, mahali padogo pa kitalii, nao wakawaleta baadhi ya jamaa mle ndani, ndipo mwongozaji mwenyewe akapotea, naye alikuwa akizurura huko nyuma. Akaja kwa farasi mahali tulipokuwa. Akasema, "Hamjambo . . ." Jamaa huyu ambaye alikuwa pamoja nami, Bw. Jeverez, kidogo alikuwa mtu anayenena haraka.

Akasema, "Hatujambo," kasema, "unatokaje humu?"

Akasema, "Uliingiaje humu?"

Akasema, "Kwa njia ile."

Akasema, "Haya basi, hiyo ndiyo njia ya kutokea." Kwa hivyo, njia ya kurudi tena, kwa hiyo hiyo ndiyo, hiyo tu.

17 Hebu tusome sasa katika Kitabu cha Wafalme wa Pili, katika mlango wa kwanza wa Wafalme wa Pili, vifungu viwili ama

vitatu. Halafu tunataka kuchukua so—somo na kulitumia kama somo la: *Njia ya Kurudi.*

> *Ikawa, baada ya kufa kwake Ahabu, Moabu wakawaasi Israeli.*
>
> *Na Ahazia akaanguka katika dirisha la chumba chake orofani, katika Samaria, akaugua: akatuma wajumbe, akawaambia, Enendeni mkaulize kwa Baal-zebubu, mungu wa Ekroni, kwamba nitapona ugonjwa huu.*
>
> *Lakini malaika wa* BWANA *akamwambia Eliya, Mtishbi, Ondoka,* na *ukaonane na wajumbe wa mfalme wa Samaria, ukawaambie, Je, si kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli, hata mnakwenda kuuliza kwa Baal-zebubu, mungu wa Ekroni?*

18 Halafu basi, nilimsikia Ndugu Moore, muda mfupi uliopita kwenye mawasiliano ya ndani, akisema, wala hakujua kwamba ningesoma hili kwa somo la kuzungumzia juu ya zeri. Nami ninataka kusoma hilo katika Yeremia 8:22:

> *Je, hapana zeri katika Gileadi; Huko hakuna tabibu? kwa nini basi haijarejea afya ya binti ya watu wangu?*

19 Swali: "Kwa nini? Kwa nini haijarejea afya ya watu Wangu?"

20 Sasa, ningependa kusema kwamba tuna furaha sana kuwa tukiufurahia wakati huu mkuu wa ushirika, nami ninatumaini kwamba Bwana hataruhusu mtu mmoja aingie humu pasipo kuokoka, na asiye na Roho Mtakatifu, ila atakayejazwa na Roho Mtakatifu, na kila mgonjwa aponywe. Ninatumainia tu hilo, na tunaliamini.

21 Sasa, hadithi yetu inaanza, usiku wa leo, na watu ambao, kama jana usiku, walikuwa wamemwacha Mungu. Na hilo ndilo jambo la kusikitisha kuliko yote ambalo ningeweza kufikiria, ni mtu fulani, mwaminio, aliye mbali na Mungu. Nasi tunaona hapa, ya kwamba mfalme huyu wa Samaria, Ahazia, sababu ya yeye kuwa mbali na Mungu, kwa sababu alikuwa na aina mbaya ya mafundisho, malezi mabaya. Mama yake alikuwa kafiri, naye baba yake alikuwa Mwisraeli aliyerudi nyuma, Ahabu. Na kupitia huko, hakupata malezi mazuri sana katika njia ya Bwana, ingawa kwa watu. . .

22 Na, Mungu hajawahi kujiacha Mwenyewe bila shahidi. Pia, Mungu alikuwa na shahidi katika siku hiyo, ila baba yake alimchukia shahidi huyu, nalo jina lake lilikuwa Eliya, nabii, naye mama yake alimchukia shahidi huyu, lakini hata hivyo, alikuwa shahidi wa Mungu, alisimama vile vile tu.

23 Mungu daima amekuwa na watu mahali fulani ambao anaweza kuwaelekezea na kusema, "Ndivyo hivyo." Loo, nataka kuwa miongoni mwa idadi hiyo. Nina hakika sote tunataka kuwa hapo, ndiyo shauku ya kila moyo. Tunataka kuwa miongoni mwa idadi hiyo ambayo Mungu anaweza kusema, "Hawa ni

watu Wangu. Waangalieni, wao ni mfano wa kile nilicho Mimi. Wanaakisi Maisha Yangu katika yao, wamesalimisha maisha yao, nami ninaakisi Yangu, Maisha, kupitia kwa yao." Ni jambo zuri jinsi gani! Ni...Jinsi hapana shaka inamfanya Mungu ajisikie vizuri kujua kwamba ana mtu anayeweza kumwamini, Naye alikuwa na mtu, na jina lake lilikuwa Eliya.

24 Na sasa, mtu huyu Mungu alikuwa amembariki, sio siku zote baraka za kimwili zinamaanisha ya kwamba uko—uko sawa na Mungu, maana Yeye aliwafanya waovu kufanikiwa. Lakini mtu huyu alikuwa—alikuwa amechukua nafasi ya baba yake, kifo cha baba yake, naye Ahazia alikuwa amemtangulia, naye alikuwa akienenda sawasawa na baba yake, na mama yake, akimwasi Mungu.

25 Naye akaanguka kupitia dirisha la nyumba yake, akaugua, labda, labda ilimponda ndani, anavuja damu ndani, au—au ugonjwa fulani ukaingia, labda maambukizi kutokana na kuanguka kwake, huenda mbavu zake zilivunjika, ama mapafu yake yakatoboka, ama chochote kile, hata akawa mahututi. Ndipo hakujua kama ataishi ama la, na kwa hiyo, badala ya kwenda, kufanya aliyopaswa kufanya, akatuma wajumbe fulani, labda mlinzi wa ikulu aliyemwamini, akawatuma mpaka Ekroni, kwa huyo mungu, Baal-zebubu, ibilisi, mpiga ramli kule, kuuliza kama ataishi ama la.

26 Sasa, hilo lingekuwa jambo la jeuri jinsi gani kwa mtu, ambaye alikuwa mfalme juu ya, waliodhaniwa kuwa, watu wa kiroho, watu waliomwamini Mungu, na hata hivyo, kiongozi wao mwenyewe akishauriana na kitu kingine mbali na kitu alichopaswa kushauriana nacho. Mnaona? Alipaswa kujua... Alijua torati, kulikuwa na makuhani nchini, kulikuwa na makanisa, na kadhalika, na kulikuwa na nabii aliyekuwa na Neno la Bwana. Na badala ya kufanya hivyo, alitaka kupitia njia maarufu zaidi.

27 Nafikiri hiyo ndiyo shida siku hizi, tunataka njia hiyo—hiyo maarufu zaidi. Naye Mungu anapofanya njia, watu humwondokea, na Mungu hufanya njia ya watu kumrudia, kama nilivyokuwa nikizungumzia jana usiku, nao watu wanakataa kufanya hivyo, basi Mungu anauliza: "Kwa nini?" Daima Yeye huuliza hilo, "Kwa nini hamkurudi?"

28 Kwa hiyo, kama akifanya njia nasi tukatae kurudi, basi—basi anauliza ni kwa nini hatukufanya hivyo. Nami afadhali nilirekebishe huku juu, kuliko kumngoja Yeye aniulize kwenye ile Hukumu ni kwa nini sikufanya hivyo. Mimi...Dhambi za watu wengine huwatangulia, wengine zinawafuata, nataka zangu zinitangulie, zimeungamwa. Halafu basi, na—nataka kuwa sawa wakati huo utakapokuja.

29 Kama vile maskini mzee ndugu mweusi alivyosema, "Mwajua, muda mrefu uliopita," kasema, "nilinena na Bwana,

nikamwambia nilitaka njia yangu iwe wazi. Sikutaka matatizo, nitakapofika kule mtoni." Kwa hivyo, nadhani kidogo ndivyo sote tunavyojisikia, hilo kidogo linalielezea, kwamba hatutaki matatizo yoyote mtoni, kwa sababu utakuwa ni wakati wa msukumano, kupigana vikumbo kubaya sana, wakati huo. Kwa hiyo, tunataka kuhakikisha kwamba tuko sawa.

30 Sasa, mfalme huyu, kulikuwa na njia iliyoandaliwa ya kujua kutoka kwa Bwana, lakini akaikataa. Ndipo Mungu akachukua njia Yake iliyoandaliwa, ambayo ilikuwa ni nabii Wake, na. . . Labda mfalme hata hakumfikiria huyu jamaa mwenye masharubu, na upara ambaye hakupendwa sana miongoni mwa watu. Ujumbe wake daima ulikuwa wa kuhukumu, na kuuma, na kupiga kumbo, na. . . watu waliokuwa karibu, kwa maana asingeweza kufanya lolote lingine, yeye alikuwa nabii. Neno la Bwana humjia nabii, naye nabii hana budi kusimama juu ya Neno, ndipo Neno lisipotiiwa, hakuna la kufanya ila kukemea. Ni hayo tu. Kwa hiyo, jamaa huyu hakumaanisha kuwa mbaya, ilibidi tu kulifanya, kwa sababu hakutawaliwa na mawazo yake mwenyewe, alitawaliwa na Roho wa Mungu.

31 Na hivyo ndivyo sote tunavyopaswa kuwa, kutawaliwa na Roho wa Mungu. Na kama tumetawaliwa, kisha tuone dhambi, inatuchefua, kuna jambo fulani kuihusu, hata iliuhuzunisha moyo wa Mungu wakati mmoja kwamba alimwumba mtu, kwa maana dhambi ilikuwa mbaya sana duniani.

32 Sasa, kwa hiyo, akauliza. . . Mungu alikuwa na njia ya yeye kujua, lakini hakuchukua njia hiyo, alichukua njia maarufu zaidi iliyokuwapo miongoni mwa watu. Na mimi—mimi nachukia kusema hivi, lakini sikuzote tunaona wito, "Marekani imrudie Mungu," "Saa ya Kumrudia Mungu," na mambo kama hayo, lakini jambo ni kwamba, wanataka kurudi kwa njia ambayo mwanadamu amefanikisha kwao kurudi. Wanataka kurudi kwa njia ya mawazo yao wenyewe, njia yao wenyewe ya kutenda, na kwa kawaida ni kinyume na njia ya Mungu ya kurudi. Ndipo basi, wanapoikataa njia ya Mungu iliyoandaliwa kwa ajili yao kurudi, basi wao. . . Mungu anawauliza, "Kwa nini? Kwa nini mlifanya hivyo?"

33 Sasa, kama tunavyoukumbuka ule wa—wakati sasa, ninii. . . ilikuwa kwamba marais wangesema, "Tutaitisha da—dakika kumi na tano za maombi," mitambo yote ilisimama. Hilo halitafanikiwa kamwe, haina budi kuchukua kuvunjika, haina budi kuchukua kufa kabisa, haina budi kuchukua kuzaliwa upya. Haichukui saa moja ya maombi, inachukua *hata* utakaporudi. Ni kurudishwa, kurudi kwenye kweli za imani, na kurudi si hata kwa. . . kwamba si jambo unalowazia, wala tangazo la kanuni za imani, au—au baadhi ya ninii, kutumia nguvu fulani za mwanadamu, bali ni kupitia kumjua Kristo Mwenyewe, kumjua Yeye, si hata Neno. Yeye. . . Kama unamjua,

unalijua Neno, kwa sababu Yeye ni Neno. Ndipo inakubidi kurudi kwenye ukweli huo.

34 Mungu anataka kujidhihirisha Mwenyewe kupitia watu Wake, nalo kanisa linataka kujidhihirisha kwa watu: idadi kubwa zaidi, umati mkubwa zaidi, watu matajiri zaidi, kadhalika namna hiyo, waliovalia nadhifu zaidi. Hilo ndilo lililotuingiza kwenye machafuko tuliyomo, tungekuwa afadhali zaidi kama sote tungalivaa magunia, ingekuwa bora zaidi kama hatukuwa na kazi, tukitembeleana nyumbani, na—na kuona kama tunaweza kupata chakula. Afadhali niwe... nilione kanisa katika hali hiyo, na hata hivyo limejazwa Roho, kuliko kuliona limeng'arishwa vizuri na kupambwa, na mambo makubwa, halafu linakufa katika Roho.

35 Mungu hufanya njia, nasi tunaikataa, haturudi kwa njia ambayo alituandalia kurudia. Naye Hezekia akafanya jambo lilo hilo, alikuwa kama wengi wetu siku hizi, alikuwa mkaidi sana, kamwe hakutaka kufanya hivyo (hata hivyo alijua Eliya alikuwa huko nyikani, alijua ya kwamba kulikuwa na Mungu Mbinguni, ila alitaka kuchukua njia iliyo maarufu sana, aende mahali ambapo watu wote, kupitia kwa nabii mke waliyekuwa naye kule, yule, mke wa Ahabu, Yezebeli, naye alikuwa kafiri, nao walitaka kwenda mpaka Ekroni, na kushauriana na mojawapo ya sanamu hizo, kama angerudi), kwa sababu akiwa mfalme, kama angejishusha chi—chini, angechukiwa na watu. Hiyo ndiyo shida.

36 Hiyo ndiyo shida, jinsi wanawake wetu wanavyofanya siku hizi. Hiyo ndiyo sababu wanaume, ukizungumza kuhusu Ukristo, wanasema, "Mimi ni wa *hiki na hiki*." Hilo halina uhusiano wowote nalo. "Ni—ninaweza kuwa mwanachama wa shirika *fulani*," hiyo bado haimaanishi wewe ni Mkristo. Ukristo haujumuishi kujiunga na kitu, Ukristo unajumuisha fa—familia, kuzaliwa katika familia, wewe ni Mkristo kwa kuzaliwa.

Lakini ni maarufu zaidi kusema, "Mimi ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Mpentekoste, ama chochote kile, mimi—mimi ni *hicho*."

37 Katikia kusema, "Mimi..." kusema, "Nimezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu amekuja juu yangu, nami ni kiumbe kipya katika Kristo": hiyo ndiyo—hiyo ndiyo njia.

38 Lakini huyo mfalme alitaka kuwa maarufu, na hivyo ndivyo watu wanavyolichukulia siku hizi. Nao wanaweza kuweka miamsho kote nchini, na kuwa na wito wa "milioni moja zaidi katika miaka *kadhaa*," au kuongeza uanachama wao na usomi wao na *kadhalika*. Wala kamwe haitaweza, kamwe... Unaenda mbali zaidi wakati wote. Njia ya kurudi, Mungu anayo njia ya kurudi. Ninataka kuzungumza nanyi kuhusu njia hiyo ya kurudi,

nawe huna budi kurudi kwa njia ambayo Mungu alikuwekea ya kurudi.

39 Sasa, hebu tuzungumzie haya. . .mfalme huyu kwa muda kidogo tu. Sababu ya kukataa, ni kwa kuwa alikuwa mkaidi. Kamwe hakuninii. . .Alitaka tu kuwa kama watu wengine. Alikuwa na njia zake mwenyewe, na alitaka kuwa hivyo, naye alitaka kuwa. . .kurudi kwa njia maarufu. Wala, hakutaka kuchukua njia ambayo Mungu alimwekea, kwa hiyo alimpuuza tu nabii huyo, na kile nabii angesema kwa sababu, bila shaka, nabii angemkemea vikali, "Tubu. Jiweke sawa na Mungu, hufai kuwa mfalme." Na loo, jinsi hiyo ingeyashusha manyoya yake chini mbele ya watu, mnaona, kama mfalme. Loo, jamani, naam, asingeweza kuvumilia hilo.

40 Kwa hiyo, labda ibilisi kule, pamoja na—na ile sanamu angesema, "Loo, Mfalme mkuu, Dk. *Nanii*, wewe ni ninii tu. . . " Mnaona? Anaweza kuwa maarufu miongoni mwa watu na kuwa na jina kuu, maarufu. Loo, jinsi watu wanavyopenda sifa za mambo. Na kwa hiyo, alifikiri kama angeweza kupata hiyo, mbona, angejitokeza mbele ya watu, angekuwa mtu aliyeadibika mbele ya watu. Basi, natumaini mnasoma katikati ya mistari kile ninachomaanisha. Kwa hiyo basi, alifikiri angekuwa mtu mashuhuri basi. Lakini asingeshuka amwendee mtu huyo ambaye angemwambia ukweli, naye kwa kweli alidhani alikuwa akimfunika kwa kitu fulani. Kwa hiyo, akawatuma watumishi. Akasema, "Nendeni mkaulize kwa mungu wa Ekroni, Beelzebubu, kama nitapona ugonjwa huu au la."

41 Naye Bwana Mungu anajua moyo wa kila mtu, anajua nia. Basi akasema. . .Huwezi kumficha Mungu chochote. La, bwana. Akasema, "Nenda kule barabarani ukakutane naye, kisha umwulize kwa nini anafanya jambo kama hilo. Je, ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli? Je, ni kwa sababu hana nabii? Je, ni kwa sababu mambo haya hayapo? Basi, kwa nini angeenda na kufanya jambo kama hilo, huku yeye ni Mwisraeli?"

42 Nashangaa kwa nini wanaume na wanawake wanajaribu kuwatenga watu katika ushirika wa—wa dhehebu, badala ya kuwarudisha kwenye msingi wa asili. Mungu anajua kuhusu hilo, lakini ndiyo njia maarufu zaidi. "Mimi ni wa *hiki-na-hiki*. Mimi ni Dk. *Nanii* kutoka katika shirika *fulani-fulani*. Ninatoka Purdue. Ni—nina elimu ya *hiki-na-hiki*. Nilipata Ph.D. yangu, LL.D. yangu." Hilo halimaanishi chochote kwa Mungu, hata kidogo.

43 Huenda Eliya hakuwa na LL.D., au Ph.D. Kwa kweli, hatujui chochote juu yake, aliingia tu jukwaani na kuondoka jukwaani vivyo hivyo. Hatujui baba yake wala mama yake walikuwa nani, hatujui lolote kumhusu, lakini Mungu alijua habari zake. Alipata mtu ambaye angeweza kumtumia, pia alipata mtu

ambaye hakuogopa. Haijalishi, kama taifa zima linampinga, bado anaita nyeusi, "nyeusi," na nyeupe, "nyeupe."

44 Mungu, tutumie mwingine. Hiyo ni kweli. Tutumie mtu ambaye haogopi, mtu ambaye sio lazima apate heshima na sifa za wanadamu, mtu anayemtazama Mungu pekee, na anamwamini Mungu, na kusema ukweli. Mtu huyo atafanya hivyo, Mungu atathibitisha ukweli huo kuwa ni ukweli.

45 Hebu niambieni, ni mwanadamu gani angeweza kufunga mbingu katika siku za maombi yake? Je, Ekroni. . .mungu wa Ekroni angeweza kufanya hivyo? Je, mungu wa Ekroni angeweza kufanya mambo ambayo Eliya alifanya? La, hasha. Ilionyesha kwamba Mungu aliye hai alikuwa pamoja na Eliya. Lakini mtu huyu alikuwa na kiburi sana, na kujigamba, hata hakutaka kujishusha kwenye kitu kama hicho.

46 Lakini Eliya akajifunga mshipi, akapanda huko na kusimama njiani, jamaa huyu mzee aliyejaa nywele akisimama pale nje, hakuwa amevaa koti la kasisi na kadhalika, lakini a—alikuwa na uso uliojaa nywele, na labda kichwa chake chenye upara kimechomwa na jua, na nywele zake zikitokeza nje, labda ungemfukuza mlangoni pako kama alikuwa akiomba-omba, naye akaja pale na kusimama barabarani namna hiyo. Biblia ilisema alikuwa amejaa nywele mwili mzima, naye alikuwa amejizungushia kipande cha ngozi, hiyo haikuwa suti nzuri sana ya kasisi, lakini asingeweza kuonyesha sifa zozote za ushirika alimotoka, lakini ndugu, alikuwa nayo chini ya moyo wake, alikuwa katika ushirika na Mungu, maana alikuwa na "BWANA ASEMA HIVI." Hiyo ndiyo njia ya kurudi. Alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Hakuwa na sura nzuri, lakini chini ya maskini mwili huo uliokonda ulipiga moyo ambao Mungu aliishi ndani yake.

47 Alisimama pale barabarani akiwa amekunja mikono yake, akiwaangalia wakija, akasimama moja kwa moja njiani mwao, ndipo walipokaribia, mbona, pengine alivuka hiyo njia, akasimama pale. Akasema, "Rudi, rudi nyuma, ukamwulize, 'Kwa nini unafanya jambo kama hilo? Je, ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli? Hivi hana nabii wa kumtaka shauri kuhusu mambo haya?' Kwa sababu amefanya hivi, mwambie 'BWANA ASEMA HIVI, hatatoka kwenye kitanda hicho.'"

48 Loo, jamani! Mungu atafanya kazi kwa njia Yake, licha ya chochote ambacho mtu mwingine yeyote anaweza kufanya juu yake. Mungu atafanya jambo hilo, atalifanya kwa njia Yake Mwenyewe. Hatutalikomesha hata kidogo, hata hatutalizuia. Ni hayo tu. Atafanya hivyo kwa vyovyote vile. Atakuwa na Kanisa, sijali ni nani asemaye hatakuwa nalo, na ni wasioamini wangapi watainuka, Mungu atakuwa na Kanisa lisilo na doa wala kunyanzi, litakuwepo. Amekwisha sema atakuwa nalo. Ah, acheni tujitahidi tu kuwa sehemu yake. Ni hayo tu. Anaweza

kutuma wahubiri kote nchini kuhubiri, kila mtu anaweza kuwakataa, awatupe gerezani, awafukuze mjini, Yeye atakuwa na Kanisa hata hivyo. Kama Yohana wa kale alivyosema, “Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Mungu angali ni Mungu. Anaweza kufanya . . .

49 Alimchukua maskini Paulo, ambapo ka—kanisa, katika uamuzi wao, lilikuwa limekosea, katika, kumchagua Mathiya, lakini Paulo huyo, maskini Myahudi mdogo mwenye pua iliyopinda, mwenye hasira kali, Yeye alisema, “Nitakuonyesha kile nitakachomfanyia.” Alimfanya mmoja wa mitume wakuu kuliko wote, kwa maana ilikuwa ni kazi ya Mungu kufanya jambo fulani.

50 Sasa, tunamwona nabii huyu akizungumza katika Jina la Bwana na kumrudisha. Ndipo mfalme akasema, “Ni mtu wa aina gani aliyewasimamisha?”

Kasema, “Alikuwa ni mtu wa ajabu-ajabu” kasema, “alikuwa amejaa nywele, na alikuwa amejifunga kipande cha—cha ngozi kiunoni mwake.”

51 Akasema, “Huyo alikuwa ni Eliya Mtishbi.” Alijua kwamba nambari yake ilikuwa imeitwa, alijua kulikuwa na kasoro. Wakati huyo Eliya aliporudi na kusema, “Mwambie ‘BWANA ASEMA HIVI, hatatoka katika kitanda hicho,’” loo, jamani, hilo lilitosha.

52 Watu siku hizi wanajiuliza. Ni kama tu m—mgonjwa aliyelala kwenye vipandio vya daktari wakati daktari ana dawa za ugonjwa wa huyo mgonjwa, naye huyo mgonjwa akatae kunywa dawa hiyo kwa chanjo yake. Pia, anaweza kuwa karibu sana na hiyo tiba mpaka ataketi moja kwa moja kwenye vipandio vya mlangoni pa daktari na afe, ni kwa sababu anakataa tiba.

53 Na ni jambo lile lile kanisani. Sasa, wao huketi moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa na kufa wenye dhambi, wanakufa wasioamini. Sio kwa sababu hakuna tiba, kuna Zeri katika Gileadi, lakini ni ukaidi wa watu wenyewe. Roho Mtakatifu yuko kwa wingi, lakini watu ndio hawamtaki.

54 Yesu alisema wagonjwa wanahitaji daktari, lakini vipi kama daktari akija na wagonjwa wasimkubali daktari? Basi daktari atafaa nini? Tunahitaji Daktari, naye mgonjwa anahitaji kunywa Dawa Yake, maana huu ni ulimwengu mgonjwa, na Kanisa gonjwa wakati wa ugonjwa. Kweli.

55 Kwa hivyo, kama mgonjwa akifa ameketi kwenye vipandio vya mlangoni pa daktari, sasa huwezi kumlaumu daktari kama atathibitisha kuwa ana dawa mle ndani za hiyo tiba, anazo dawa mle ndani kwa ajili ya—kwa ajili ya ninii yake . . . tiba kwa ajili ya uponyaji wake. Naye huyo mgonjwa anaketi kwenye hivyo vipandio, “Sasa, siingii humo ndani.” Mbona, humo ndani ndiko kwenye tiba!

56 Vema, una ugonjwa *fulani*. Mbona, ana kabati iliyojaa dawa ambazo zitauangamiza ugonjwa huo, ni dawa ya sumu ambayo itaondoa ugonjwa huo. Hawa hapa wengine, waliponywa, waangalieni. Walikuwa na ugonjwa huo, wala hawanao tena. Na daktari ana dawa nyingi, nawe unakwamia kwenye hivyo vipandio na kusema, "Vema, nimekuja umbali huu, endapo anataka nipone, atatoka hapa nje na kulishughulikia." Loo, la. La, la. Hivyo sivyo. La, utafia kwenye hivyo vipandio, wala haitakuwa kosa la daktari, wala haitakuwa ukosefu wa dawa, ni kwa sababu ya ukaidi wa watu wenyewe ambao hawatakunywa dawa.

57 Nalo Kanisa ni vivyo hivyo. Tunayo Maandiko mengi, tuna Jambo litakalolinyoosha Kanisa, tunacho Kitu kitakachowarudisha mahali mlipokuwa miaka hamsini iliyopita, lakini hamna budi kutaka kukichukua, hamna budi kutaka kuponywa, Tiba ya magonjwa haya, magonjwa haya ya kiroho, hamna budi kuwa Nayo.

58 Sasa, ni jambo la hatari. Tulikuwa nayo katika nchi yetu, sasa hivi, hiyo chanjo ya Salk, walimwomba kila mtu achanjwe, wote vijana kwa wazee, wachanjwe polio hii ya kutisha, na kila mtu, maelfu waliingia wakachanjwe. Nao wa—walifanyaje hilo?

59 Mnaona, mnaona katika kutumia dawa za daktari, mnajua zitafanya kazi kwa baadhi ya watu, halafu hazitafanya kazi kwa hao wengine, kwa sababu kwamba, mnajua, kila mtu hajaumbwa kwa namna ile ile. Sasa, tuna penisilini hii, mimi hubeba kadi mfukoni mwangu, ili kwamba kama kamwe nikipata ajali, kamwe daktari hapaswi kunipa penisilini, ingeniua. Kwa hiyo, itawaua baadhi ya watu na kuwasaidia wengine, kwa sababu chanjo hii haifanyi kazi sawa kwa watu wote.

60 Umewahi kufikiria, jinsi wanavyoipata chanjo, jinsi wanavyoifanya? Wanasoma vitabu, na wanakemia wanakwenda na kuchukua vijidudu fulani, nao wanavichanganya, na sumu mbalimbali, mpaka wapate fomula, kitu ambacho hakitamwua mgonjwa, bali kitaua hicho kiini, na hivyo ndivyo wanavyofanya kazi. Ndipo wanavikusanya vyote hivi pamoja, kisha wanaenda wanamchukua nungubandia, kisha wanachukua sindano ndefu, nao wanamdunga huyo nungubandia, na kummiminia yote, ndipo basi, kama huyo nungubandia akipona hiyo, basi wanakudunga wewe, waone kama utapona hiyo. Vema sasa, hiyo ni sawa, wamefanya mambo makuu, mnaona, katika kufanya hivyo, lakini hivyo ndivyo wanavyojua jinsi ya kuwafanyia watu.

61 Sasa, mnaona ya kwamba kila mtu hajaumbwa kama nungubandia, kwa hiyo ha—haitumiki kwa kila mtu. Lakini nataka kuwaambia jambo moja: chanjo ya Mungu hutumika kwa

kila mtu, Itatumika kwa kila mtu, Hiyo ita—Hiyo itasaidia kila mtu anayeipokea.

62 Naye Mungu anauliza swali, "Je, hapana Zeri katika Gileadi, au hakuna Tabibu huko? Basi ikiwa iko, mbona haijarejea afya ya binti ya watu Wangu, ugonjwa, maradhi, ya binti Yangu?" Hilo lingekuwa ni Kanisa, "binti ya watu Wangu," ambapo, Kanisa la Kiorthodoksi, Yeye alikuwa akizungumza nasi moja kwa moja. "Binti ya watu Wangu hajapona ugonjwa wake. Je, ni kwa sababu hatuna Tabibu, au hatuna—hatuna. . . Hana dawa ya kutumia, hana zeri, hakuna Tabibu?"

63 Sasa, tunaambiwa na sayansi ya matibabu siku hizi, ambayo tunaipongeza sana kwa mambo haya, kwamba kama tuna magonjwa haya mbalimbali na tukose kupata chanjo hizi, ni jambo la hatari, unaweza kupoteza maisha yako usipoipata.

64 Tunaishi katika siku za—za dhambi na magonjwa. Tuna magonjwa mengi kuliko tuliyowahi kuwa nayo, kwa sababu kuna dhambi nyingi na—na kadhalika kuliko tulizopata kuwa nazo, hilo ndilo chimbuko la magonjwa, magonjwa ni matokeo ya dhambi. Kabla ya kuwa na ugonjwa wowote hatukuwa na dhambi, nayo dhambi ilifuata ugonjwa, mnaona, ninamaanisha, ugonjwa ulifuata dhambi, kunradhi. Walikuwa na dhambi kwanza, nayo matokeo ya—ya dhambi yakasababisha magonjwa. Sasa, na kwa hiyo, sasa, dhambi inapoongezeka, ugonjwa unaongezeka. Nasi tuna madaktari bora sana tuliowahi kuwa nao, tuna dawa bora kuliko tulizopata kuwa nazo, tuna hospitali nyingi kuliko tulizowahi kuwa nazo, tuna watu waliofunzwa vizuri kuliko tuliowahi kuwa nao, nasi tuna magonjwa mengi kuliko tuliyopata kuwa nayo. Kwa nini? Tuna dhambi nyingi kuliko tulizowahi kuwa nazo. Tunao watu wengi zaidi, nao watu wanapoanza kuongezeka, ndipo dhambi na vurugu zinaingia.

65 Miji hii mikubwa, si kama kuishi mashambani, miji iliyozungushiwa kuta ambayo tulizungumza juu yake jana usiku, ukichukua miji hii yenye kuta, sikuzote unapata dhambi. Na tunapopata aina hii nyingine ya miji ya kiroho iliyozungushiwa kuta, sikuzote unaichanganya na kila kitu, dhambi pia.

66 Sasa, tunaona, madaktari wanatwambia kwamba muuaji namba moja ni ugonjwa wa moyo. Kweli, sipingani na daktari, kwa sababu mimi si daktari, lakini nasema jambo moja, muuaji namba moja sio ugonjwa wa moyo, muuaji namba moja ni tatizo la dhambi. Dhambi ndiyo muuaji namba moja, sio ugonjwa wa moyo.

Wengi sana siku hizi wanasema, "Unajua, Ndugu Branham, u—u—unasema mambo haya kwa ukali sana, hatuna budi kutenda dhambi kidogo kila siku, hatuna budi tu."

67 Mtu fulani anasema, "Unajua, Ndugu Branham, ninakusikia ukilaani uvutaji sigara," nami kweli naamini kwamba watu

hawapaswi kuvuta sigara, ninaamini katika utakatifu, usafi, kotekote, nafsi, mwili, na roho, naye akasema, "sisi . . . inanibidi tu kuvuta sigara. I—inanibidi tu kuvuta sigara kidogo, inanibidi tu kuivuta."

Halafu tunawasikia wengi sana wanaosema kwamba "Sina budi kunywa pombe kidogo ya kijamii kusudi niidumishe kazi yangu."

68 Tunasikia wanawake wakisema, "Inanibidi tu kukata nywele zangu na kuvaa nguo zangu za kisasa ili kudumisha hadhi yangu ya kijamii kanisani mwangu, nisipofanya hivyo, wanawake wanasema ninaonekana mkongwe sana."

69 Samahani, lakini nitasema jambo fulani: Huo ni ukahaba wa Kipentekoste. Hiyo ni kweli. Sababu ya wao kufanya hivyo ni kwa sababu hawajaijaribu ile chanjo. Hawajaijaribu Chanjo ya Mungu kwa ajili ya dhambi na mambo haya. Hiyo ni kweli.

70 Sasa, nitawaambia tu njia ya kurudi. Je, mnataka kurudi? Hamna budi kuchanjwa. Huna budi kuchukua Zeri ya Mungu, Chanjo ya Mungu. Yeye anayo, ni Tiba maradufu ya dhambi: Damu ya Yesu Kristo. Mwana wa Mungu Mwenyewe, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, hukusafisha na dhambi na kukujaza kwa ajili ya huduma. Hivyo ndivyo inatubidi kurudi, ni kupitia vipengele hivyo hapo. Sio lazima ufanye mambo hayo, sio lazima uyafanye. Na sababu yenyewe ya wewe kufanya hivyo . . .

71 Mhudumu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, akasema, "Ndugu Branham, kweli ninaamini kwamba ubatizo huu wa Roho Mtakatifu unaozungumzia ni wa kweli, kweli naamini hivyo." Akasema, "Kanisa langu linafundisha ubatizo wa Roho Mtakatifu, lakini tunaamini tunampokea Roho Mtakatifu tulipoamini, mara tunapoamini, kwamba Ibrahimu alimwamini Mungu, na yeye, ikahesabiwa kwake . . . ikahesabiwa kwake kuwa haki."

72 Nikasema, "Hiyo ni kweli, lakini basi Mungu akampa muhuri wa tohara kama thibitisho la imani yake." Nikasema, "Kama bado hujampokea Roho Mtakatifu, Mungu hajawahi kuitambua imani yako." Hiyo ni kweli. Sisi ni wana wa Ibrahimu.

Akasema, "Kama ningefanya hivyo, hata hivyo, Ndugu Branham, kama ningefanya hivyo, basi ningefukuzwa kanisani mwangu."

Nikasema, "Kwani kuna nini? Mimi nilifukuzwa."

Naye akasema, "Naam mimi . . ." kasema, "Naam, siwezi kufanya hivyo."

Nami nikasema, "Kwa nini huwezi kufanya hivyo? Niambie tu kwa nini huwezi kulifanya."

Akasema, "Vema—vema, nisingeweza kupata mikutano mingine mahali popote."

73 Nikasema, "Upuuzi. Kama Mungu anakuitia Injili, ana mahali pako pa kuhubiria, ana mtu ambaye atakusikiliza. Hakika. Kutakuwa na mtu ambaye atasikiliza; simama pembeni mwa barabara."

Kasema, "Watanitupa gerezani."

"Basi mhubirie mlinzi wa gereza," hiyo ni kweli, "mtu fulani." Paulo alifanya hivyo, wote wakaokoka. Naam, bwana.

74 Unasema huna budi kufanya hivyo. La, haikulazimu. Sababu ya wao kufanya hivyo, ni kwa sababu hawajaijaribu chanjo hii, bado hawajakunywa Sumu bado kwa ajili yake. Kuna kitu Fulani kitakachoutibu huo, kitakachotibu hofu hiyo uliyo nayo, kuna kitu Fulani kitakachokufanya uvae na kutenda kama mama wa heshima, kuna Kitu kitakachokufanya uishi kama Mkristo, kuna Kitu kitakachokufanya—kitakachokufanya ujazwe sana na Mungu mpaka usimame na kutoa ushuhuda utakaovitikisa viezekeo kwenye paa la nyumba, ikiwa tu utachanjwa, lakini huna budi kunywa hiyo Sumu.

75 Una ugonjwa, kwa hiyo kuna jambo moja tu la kufanya, ni kunywa Sumu uuondoe. Hiyo ndiyo njia ya kuirudia afya ya kawaida ya Kikristo. Kanisa linaugua, ni dhaifu, limepungukiwa na damu, lina ugonjwa mbaya, wala halina tiba ya duniani; elimu haitasaidia, tumeijaribu; dhehebu halitasaidia, tumelijaribu, utauzorotesha tu zaidi. Kuna njia moja tu ya kurudi, na hiyo ni kupitia kwa Damu ya Yesu Kristo, chanjo. Mrudieni Kristo, mrudieni Roho Mtakatifu, urudieni Uzima wa Milele tena. Hiyo ndiyo njia tungerudia.

76 Watu wanasema, "Sina budi kufanya hivi ili kudumisha hadhi yangu kwa watu." Sio lazima ufanye hivyo, inaonyesha uhaba wa umakini, inaonyesha woga, naye mhubiri ambaye atasimama mimbarani na kupatana juu ya kanuni za Kristo kwa sababu kundi fulani la maaskofu wanamtawala na kumwambia, "Inakubidi kufanya hivi, la sivyo tutakufukuza katika ushirika," wewe ni mwoga. Simama hapo, sema ukweli, haidhuru inagharimu nini.

77 Mwangalie Stefano asubuhi ile, ndugu yetu mdogo wa Roho Mtakatifu, amesimama mbele ya Baraza la Wazee, mlango wa 7 wa Matendo, akasema, "Enyi watu wa Israeli, ninyi mkaao Uyahudi," na kadhalika, "jinsi baba zetu walivyopanda kutoka Mesopotamia," na kadhalika, akaanza kuwaambia, ndipo akachochewa, akaanza, Roho Mtakatifu akaja juu yake, akasema . . . aling'aa, uso wake ukang'aa kama Malaika, akasema, "Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa mioyo wala masikio, sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu, kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo." Whiu! Hmm. Alijua mahali alipokuwa amesimama, alijua msimamo wake, uso wake haukuninii, huenda uling'aa kama nuru huko juu, lakini malaika anajua anachofanya; naye malaika ni mjumbe aliyeagizwa

kutoka kwa Mungu, si lazima ayaandike, yeye anajua kabisa. Hao mbwa-mwitu nusu milioni wa makasisi wanaobweka wakimhukumu mtu huyo, jinsi alivyokuwa akitenda na mahubiri aliyokuwa akihubiri, ndipo Stefano akasimama pale na kusema, “Hamjatahiriwa moyo wala masikio, nanyi mnampinga Roho Mtakatifu, kama baba zenu walivyofanya, vivyo hivyo mnafanya jambo lile lile.” Alikuwa akiwaambia njia ya kumrudia Mungu aliyeifungua Bahari ya Shamu, au kuwaambia, kwa Mungu aliyeyanyesha yale mapigo huko Misri.

78 Lakini hawakutaka kushika njia ya kurudi, kwa hiyo wakampiga huyo mjumbe kwa mawe. Huliondoshi hivyo, lingali linadumu. Yule aliyeshuhudia alifanyika mmoja wao hivi karibuni sana, Paulo. Hiyo ni kweli. Naam. Hawajaijaribu ile Sumu.

79 Unajua sababu ya wao kufanya hivyo? Wanaogopa huko kuzaliwa kupya, ninamaanisha kuzaliwa upya halisi. Loo, kila mtu anasema, “Hakika, ninaamini huna budi kuzaliwa mara ya pili. Naam, bwana.” Ndiyo, lakini inapofikia kuzaliwa halisi, wanaamini kuzaliwa upya kwa kupeana mikono, kukariri lundo la kanuni za imani, ama *kitu kingine*, wanaita huko kuzaliwa upya. Huko sio kuzaliwa upya, wanaogopa kuzaliwa upya.

80 Sikilizeni, uzazi wowote ni mchafuko, sijali kama uko kwenye zizi la nguruwe, au uko wapi, ni mchafuko, kuzaliwa kokote, vivyo hivyo na kuzaliwa upya, kuta—kutakufanya ufanye mambo ambayo hukufikiria ungewahi kufanya, bali huleta Uzima, na kabla ya kuwa na Uzima, huna budi kuwa na mauti. Kabla ya mbegu kujizalisha yenyewe, haina budi kufa ili kwamba, wala si kufa tu, bali haina budi kuoza, ili kupata uhai mpya kutoka kwake, haina budi kufa na kuoza yenyewe. Vivyo hivyo na kila mwenye dhambi. Kila mtu, haijalishi ana elimu ya hali ya juu jinsi gani, na ameadabika kiasi gani, ana digrii ngapi kanisani, ama kadhalika, mangapi ya mambo haya, amesomea vyuo vingapi, hana budi kufa kwa nadharia yake mwenyewe, lazima aifie nafsi yake, hana budi kufa kwa kila kitu apate kuzaliwa upya na Roho Mtakatifu. Itamfanya alie, na “buu-huu,” na kunena kwa lugha, na kuruka juu chini, na kupiga makelele kama mwendawazimu, lakini amepata Uzima mpya. Hilo ndilo linalohitajika kufanya hivyo, hana budi kuwa na Uzima mpya. Wanaogopa kuzaliwa upya, kuzaliwa upya ni mchafuko.

81 Sasa, wanaita kuzaliwa upya, loo, kila kitu, “Loo, hakika, ninaamini katika kuzaliwa mara ya pili.” Nao wanasema wamezaliwa mara ya pili, na kulikana Neno? wanasema wana Roho Mtakatifu, na kuchukua Maandiko ambayo yanafundisha Biblia waziwazi, jinsi ilivyo, halafu wanasema, “Loo, *hiyo* ilikuwa kwa ajili ya wakati mwingine,” na unamaanisha kwamba Roho Mtakatifu aliye ndani yako atashuhudia *hiyo* ilikuwa kwa ajili ya wakati mwingine? wakati Yeye alisema, “Ni

kwa ajili yenu na watoto wenu, kwa wale walio mbali, na wote ambao Bwana Mungu wetu atawaita." Hawezi kusema uongo. Na, ikiwa kuna roho ndani yako anayeikana hiyo kuwa kweli, basi huyo si Roho Mtakatifu, maana Roho Mtakatifu aliandika Neno. Amina. Hiyo ni thabiti kama ninavyojua jinsi ya kuiweka.

82 Inachukua kifo kuzalisha uzima. Huna budi kufa kwa mawazo yako mwenyewe, huna budi kufa kwa theolojia yako mwenyewe, huna budi kufa kwa nafsi yako mwenyewe, kwa njia zako mwenyewe za kibinadamu; huna budi kuzaliwa upya, kiumbe kipya, uumbaji mpya. Kabla ya kuweza kuwa hivyo, huwezi kuwa wawili kwa wakati mmoja, unapaswa kufa kwa mmoja upate kuzaliwa katika Mwingine. Nako huleta mchafuko, na husababisha mchafuko pia, lakini wewe ni. . .una Maisha mapya. Je, inaleta tofauti gani? Huna budi kufanya hivyo.

83 Unajua, kulikuwa na wakati ambapo hatungeweza hata kuwachanja watu kwa ajili ya homa ya matumbo. Ninamwangalia rafiki yangu, nesi, anayeketi hapa akinitazama ninapozungumza haya, lakini hiyo ni kweli, ya kwamba, Dada Dauch, kulikuwa na wakati ambapo hawakuwa na chanjo ya homa ya matumbo, maelfu walikufa nayo. Kulikuwa na wakati ambapo hawakuwa na chanjo ya polio, maelfu mara maelfu ya watoto wadogo walikufa, lakini sasa hakuna udhuru, tuna chanjo. Hiyo ni kweli. Sawa.

84 Sasa, kulikuwa na wakati ambapo sumu hii, au zeri ambayo tutaiita sumu ya Mungu, kwamba haikuwa kamilifu sana, kwa sababu iliitwa. . .ilikuwa kwa damu ya mbuzi, na kondoo, na ng'ombe, na kadhalika. Haikuondoa dhambi kabisa, ilifunika tu dhambi. Ilimbidi mtu kwenda mwaka baada ya mwaka, kufanya maungamo yake na kadhalika. Kulikuwa na wakati ambapo ilikuwa, sawa. Lakini sasa mwabuduo, akiisha kutakaswa, hajioni tena kuwa mwenye dhambi. Nayo dhambi ni nini? Kutokuamini. Kutokuamini nini? Neno. Bila shaka. Ukisema unamwamini Mungu na kulikana Neno Lake, mbona, humwamini. Ukisema, "Ninamwamini Ndugu Branham," useme, "lakini amekosea. Yeye ni. . ." Vema, unawezaje kufanya hivyo? Usingeweza kufanya hivyo. Najua ulikosea, kwa sababu hukuniamini. Na kama ukisema unamwamini Mungu, na kulikana Neno Lake, vema basi, humwamini Mungu, maana Mungu ni Neno Lake. Kamwe huwezi kufanya hivyo, huna budi kulikubali Neno ambalo ndilo njia ya kurudi kwa Njia ya Neno, nalo Neno ni Mungu.

85 Sasa, tunaona jambo hilo. Pia, tunaona ya kwamba, wakati mmoja ambapo chanjo hiyo haikuwa nzuri sana, kulikuwa na dhamiri ya dhambi sikuzote, na ilimbidi kuja mwaka baada ya mwaka na kutoa sadaka yake. Lakini sasa, katika Waebrania, inatwambia kwamba mwabuduo akiisha kutakaswa mara moja tu, hana dhamiri ya dhambi tena, ama vinginevyo, hana tena tamaa ya kutenda dhambi, jambo hilo lote limemwondokea.

Hakuna tena...Si lazima utende dhambi kila siku, si lazima ufanye mambo haya, unafanya hivyo kwa sababu unataka kufanya hivyo makusudi. Na sababu ya kutaka kufanya hivyo makusudi ni kwa sababu hukujifia nafsi yako. Loo, ndugu, najua hilo linachoma, lakini ni zuri. Amina. Unapoifia nafsi yako basi unakuwa kiumbe kipya, ndipo mambo hayo yametoweka.

86 Na kama ukijaribu kufanya kana kwamba unayo kabla ya kuwa nayo, ni kama, nilisema hivi majuzi, kama ndege mweusi akijaribu kujivika manyoya ya tausi kwenye mbawa zake, aseme, “Mnaona, mimi ni—mimi ni tausi.” Siye. Hicho ni kitu ambacho amejibandika mwenyewe, lazima yakue kutoka ndani kwenda nje.

87 Na hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo, si kitu unachojipaka au kitu kama hicho. Ni kuzaliwa upya, huna budi kuzaliwa mara ya pili, nazo nguvu hizi za Roho Mtakatifu hazina budi kutoka ndani kwenda nje. Basi wakati ulimwengu na dhambi, na kukata nywele, na kujipaka rangi kunapotokea kinyume na Neno la Mungu, inaonyesha Roho Mtakatifu hayupo, huo ni ushahidi wa moja kwa moja. Kwa hivyo, ungeuitaje? Ukahaba wa Kipentekoste, hiyo ni kweli kabisa, kufanya uasherati wa kiroho na Mungu wa Mbinguni. Ni aibu, fedheha jinsi gani! Loo, hilo ni la kutisha! Naam, bwana.

88 Sasa, tunaona ya kwamba mwanadamu anapojaribu kutafuta dawa ya chanjo, daktari, kumpa mgonjwa wake, kumchanja kutokana na ugonjwa, kwanza anaijaribu kwa nungubandia, aone kama itafanya kazi. Lakini Mungu hakufanya hivyo, Yeye kamwe hakuchukua nungubandia, aliitumia Mwenyewe. Daktari mzuri anayetaka kujaribu dawa ya chanjo, endapo hajui kama itaua au kutibu, anapaswa kuichukua yeye mwenyewe kwanza apate kujua kabla hajampa mtu mwingine.

89 Naye Mungu, ili, kuichukua Dawa hii ya chanjo, ilibidi afanywe mwili na aishi miongoni mwetu, Mkombozi wa Jamaa. Amina. Ilibidi Mungu awe mwanadamu, ili aweze kuchukua hiyo Dawa ya chanjo. Naye alipata chanjo Yake pale Yordani, amina, alipoingia mtoni kwa Yohana na kubatizwa, na kisha Chanjo ikashuka. Sumu ikashuka kutoka mbinguni kama hua, akisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake.” Alichanjwa.

90 Na mara baada ya chanjo kuja, jaribu likaja. Basi kila mtu, mara tu unapompokea Roho Mtakatifu na kuchanjwa, kila pepo kutoka kuzimu atakushambulia. Hata familia yako mwenyewe, wakati mwingine itakukataa: mume wako, mke wako, mchungaji wako; unafukuzwa kanisani, unachekwa, unadhihakiwa; ni jaribu. Amina.

91 Mungu alifanyika mwili, mmoja wetu, apate kuchanjwa, akawa chini ya dhambi. Kwa maana alizaliwa na mwanamke,

alijaribiwa kwa kila namna kama sisi, wala asingeweza kufanya hivyo maadamu alikuwa katika Roho; ilimbidi kufanyika mwili kusudi, ajaribiwe, apate kuchanjwa, apate kuinywa ile Sumu, alitaka kuthibitisha kwamba Sumu Yake ilikuwa sahihi. Amina. Kwa hiyo aliichukua siku ile ambayo Yohana alimbatiza wakati ile Sumu iliposhuka kutoka Mbinguni na kumjaza.

92 Kisha jaribu likaja. Ilishikilia katika kila jaribu la dhihaka, ilishikilia wakati Shetani alipomtolea falme za ulimwengu, apate kumpa ulimwengu, na kila ufalme, hiyo chanjo ilishikilia, ilikaa imara. Ulimwengu ulimtazama, kanisa likamtazama, wakosoaji wakamtazama, ibilisi alimwekea kila jaribu aliloweza, nayo ingali ilishikilia. Amina.

93 Aliposimama mbele ya kundi lile la makuhani wenye elimu, Yeye alisema, "Ni nani kati yenu anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi?" Amina. Chanjo hiyo ilishikilia hapo. "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini. Bali nikizifanya kazi za Baba Yangu, basi ziamininі hizo kazi."

Wakasema, "Wewe ni mwanadamu unayejifanya Mungu."

94 Akasema, "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiamini." Kasema, "Hizo ndizo zinazonishuhudia Mimi, zinanena habari Zangu, matendo Yangu yanena kwa sauti kubwa kuliko kinywa Changu kiwezavyo."

95 Hiyo ni kweli kabisa. Wewe ni kile ulicho kwa jinsi unavyoishi. Wewe si kile ulicho kwa jinsi unavyoongea, au jinsi unavyovalia, au jinsi ulivyo, jinsi unavyoishi, hicho ndicho kinachokufanya ulicho. Upande wa nje huonyesha kilicho ndani. Kizazi hiki kitupu, kisicho makini, kinachocheza karata, kinachovuta sigara ambacho hujiita Wakristo, wanawake waliokata nywele, wacheza dansi, wazimu wa televisheni, mizaha michafu, mnaojiita Wakristo, mnahitaji chanjo. Rudini kwenye Pentekoste tena! Hiyo ni kweli. Tuna upungufu mkubwa.

96 Ilishikilia kwa Yesu wakati Yeye alipojaribiwa kwa kila kitu ambacho mwanadamu angeweza kujaribiwa kwacho, kila jaribio lililowahi kumwangukia mtu lilimwangukia Yeye, lakini chanjo hiyo ilishikilia. Ukitaka kujua kama itashikilia au la, kama jambo hili ni la kweli au la, mwangalie Yeye, Yeye alikuwa Mfano wako. Ilishikilia Kwake, ilishikilia kwa kila jaribio; ilishikilia wakati aliposimama pale na angeweza kutambua mawazo ya watu, nao wakamwita Beelzebuli, halikumzuia, aliendelea moja kwa moja vivyo hivyo.

97 Alipoyajua mawazo ya mioyo yao, alipoangalia huko nje na kumwambia yule mwanamke kisimani kwamba alikuwa na waume watano, akamwambia Petro jina lake lilikuwa nani, na kadhalika, wao wakasema, "Mtu huyu ni mpiga ramli."

Sasa, Yeye hakusema, "Vema, labda nimekosea. Lab-. . . " Ilishikilia! Kwa nini? Alijua alikotoka.

98 Niliwauliza wanafunzi wangu hivi majuzi, tulipokuwa tukihubiri kwenye wa pi-. . ., au, mlango wa 3 wa Yohana Mtakatifu, nikasema, “Nitawaacha mkishikilia hili, hadi mkutano unaofuata: Yesu aliposimama hapo na kusema, ‘Hakuna mtu aliyepaa juu ila Yeye. . .juu Mbinguni, ila Yeye aliyeshuka kutoka Mbinguni, ndiye Mwana wa Adamu aliye Mbinguni.’” Hilo linahitaji chanjo. “Hakuna mtu aliyepaa Mbinguni, ila Yeye aliyeshuka kutoka Mbinguni, ndiye Mwana wa Adamu ambaye sasa yuko Mbinguni,” Naye huyu hapa alikuwa amesimama, akizungumza na Nikodemo. Kanisa, wanadorora, wanalipuuza takriban saa chache, mara wanaliacha. Nilisema, “Ilithibitisha Yeye alikuwa Mungu, Yeye yuko kila mahali.” Hiyo ni kweli kabisa. Hakika. Alichanjwa. “Si Mimi nizitendaye kazi hizi. Ni chanjo Yangu, Baba Yangu akaaye ndani Yangu, Yeye Ndiye anayezitenda kazi. Na kazi nizifanyazo,” Yohana Mtakatifu :12, nne-. . . “yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” . . .?. . .

99 Kwani makanisa yana shida gani? Kuna shida gani leo, wanaweza kulihukumu, waseme ni la ibilisi? Hawajachanjwa bado, hawajui ile Dawa ya chanjo ni nini. Hiyo ndiyo sababu, ni kutokuamini, na kutokuamini ni dhambi. “Yeye asiyeamini amekwisha hukumiwa tayari.” Kutokuamini ndiko kunakofanya hivyo.

100 Ilishikilia. Walienda wakamfunika kitambaa usoni. Sasa, Mtu aliyekuwa na nguvu za kufanya mambo haya. . .Hiyo ndiyo shida na mwenendo wetu wa Kipentekoste. Nisikilizeni, nitasema jambo fulani, si kuudhi, bali kutibu. Mtu anapokuja kwako ambaye ana ujanja unaoweza kujibu kila moja la maswali yako, sahau hilo. Kila mtu, anayeweza kukwambia kila tafsiri ya ndoto, anayeweza kuponya kila ugonjwa, anayeweza kufanya mambo haya yote, na jamani, yeye ni mtu mwenye kitu kinachoweza kufanya mambo yote, hayo ni kinyume na Neno, ana jibu la kila kitu, ni kinyume na Neno. Wewe zingatia hilo.

101 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, ni watu wanaochochewa sana, nao wanaenda kombo kwa hisia za kimwili, na kuweka tafsiri kwa mambo wakati si tafsiri. Nimechefushwa sana nalo, nikipitia nchini na kusikia mambo haya, si—sitaki kuumiza hisia za mtu yeyote, lakini usiku wa leo, usiku wa leo ninawaambia njia ya kurudi, jinsi ya kurudi kwenye Tiba. Hiyo ni kweli kabisa. “Nabii akitabiri, na yale asemayo yasitimie, basi msimwamini.” Hiyo ni kweli. “Lakini kama yakitimia, mwaminini, kwa kuwa Mimi Ndiye niliyenena,” Ilikuwa ni Bwana.

102 Huyu hapa Yesu alikuwa amesimama pale, alikuwa ni Mfano wa ajabu jinsi gani! Paulo alikuwa mfano mzuri jinsi gani! Hapo alikuwa na uwezo wa kumpiga mtu kwa upofu, kuwaponya wagonjwa, kuwaita vilema wakaponywa, mambo haya yote, halafu basi, ungeweza kuwazia, sehemu ya mwisho ya huduma yake, aliposimama pale, akamwacha mfua shaba kuusimamisha

mkutano wake na kumfukuza kutoka nchini? Nadhani baadhi ya wakosoaji wanasema alipoteza uwezo wake wa kupofusha. La. La, hakuwa na vitimbi, alikuwa na Roho Mtakatifu, alimjali Mungu tu. Nadhani basi, alimwacha rafiki yake akiwa mgonjwa kule juu, Trofimo, juu mahali fulani akiwa mgonjwa, nadhani alipoteza nguvu zake za kuponya, pia aliandamana na daktari, mponyaji wa Kiungu, akiambatana na daktari, Luka. Mungu alikuwa akijiandaa kuitia taji huduma yake, maana Paulo daima alitaka kuteseka kwa yale aliyomtendea Stefano, ilikuwa ndiyo shauku yake. Hivi hamjui jinsi Roho Mtakatifu alivyonena naye, akamwambia asipande kwenda Yerusalemu? Alijua alikuwa anaenda kufa kwa ajili ya Yesu; hiyo ndiyo iliyokuwa shauku ya moyo wake, kufa kwa ajili Yake.

103 Mwangalie Yesu, ambaye angeweza kuwaponya wagonjwa, na kuwafufua wafu, na kufanya mambo haya yote, na kutabiri, na kuwaambia watu, na kuyajua mawazo ya moyo wao, ameketi barazani mwa Pilato pale, huku amefungwa kitambaa machoni Mwake *hivi*, na askari wa Kirumi, kundi la hao walevi, na mate yao usoni Mwake, na ameng'olewa ndevu usoni Mwake, wakimpiga kichwani kwa mwanzi, kisha wanapokezana ule mwanzi, na kusema, "Aisee," wanamvua kitambaa, kasema, "sasa twambie, wewe ni nabii, twambie ni nani aliyekupiga, tutakuamini." Hakufungua kinywa Chake kamwe. Hakika. Hakuwa na vitimbi, ilikuwa ni Mungu.

104 "Ondosha mikono yako msalabani na ushuke, nasi tutaamini, kwa kweli, sisi ni makuhani, sisi ni watumishi wa Mungu, kama utathibitisha tu na kushuka kutoka msalabani, mbona, tuta—tutajua ya kuwa wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ndiye mfalme wetu, shuka msalabani, nasi tutakuamini." Yeye kamwe hakufungua kinywa Chake na kusema Neno.

105 Kwa nini? Kundi hilo la wanafiki kule chini wakiimba wimbo ule ule ambao Roho yeye yule aliyekuwa ndani ya Daudi aliupazia sauti kule nyuma, "Mungu wangu, mbona umeniacha? Walinichoma mikono na miguu," Zaburi ya 22, "walilipigia kura vazi langu, wakapiga kura," na kadhalika, wakiimba wimbo ule ule kule chini ambao Daudi, kwa Roho Mtakatifu, aliulilia yapata miaka mia nane kabla ya hapo, akisema jambo lile lile, na kumsikia akiugumia, wala hawakujua.

106 Nao hawa wanatheolojia siku hizi, wanavyojiita, na madhehebu wanasoma juu ya mambo haya ya Pentekoste kule nyuma, na kuona jambo lile lile likitenda kazi, na kisha wanaliita "watakatifu wanaojibingirisha." Ni fedheha jinsi gani! Halafu tunajiita kanisa kuu la Kikristo, watu wa Kipentekoste. Ninalitilia shaka. Angalieni, si kama dhehebu hatuwezi kuwa Wapentekoste, tunaweza kuwa Wapentekoste kama watu binafsi, hiyo ndiyo njia pekee tunayoweza, kwa sababu ni tukio.

107 Sasa, walipojaribu kumfanya Yeye awaambie jambo fulani, wakati Shetani alipojaribu kusema, “Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, sasa, unajua una uwezo, geuza mawe haya yawe mkate, jisaidie Mwenyewe, umekuwa siku arobaini bila chakula, ndipo nitakuamini na kutubu,” Angeweza, kama angekuwa akimjali Shetani. Ile chanjo ilishikilia. Alijua wakati wa kuzungumza na wakati wa kunyamaza. Hiyo ndiyo shida yetu siku hizi, tunazungumza kupita kiasi wakati mwingine. Jua wakati wa kuzungumza na jambo la kusema, usiseme chochote mpaka Mungu aseme hivyo. Unawezaje kufanya hivyo? Kama hufanyi hivyo, Mungu hakwambii kibinafsi, basi unakosea, unakufuru, unapofanya hivyo. Hakikisha kabisa kwamba ni Mungu, acha Mungu anene nawe moja kwa moja, ndipo useme ni BWANA ASEMA HIVI.

108 Kama nikienda na kusema, “Jack Moore aliniambia *hivi na hivi,*” wala hakuniambia, ningekuwa nikidanganya. Loo, jamani! Tunachohitaji ni kurudi kwenye chanjo, kurudi kwenye nguvu zile za Pentekoste, kurudi kwenye Roho Mtakatifu. Naam, bwana. Tunaenda mbali zaidi nalo wakati wote; kanuni zetu za imani, na makanisa, na madhehebu yanawagawanya watu na kuwapeleka mbali zaidi wakati wote.

109 Ile chanjo ilishikilia kwa Yesu, ilishikilia pale msalabani, ilishikilia wakati angeweza kushuka kutoka kwenye msalaba huo. Billy Sunday alisema, “Kila mti ulikuwa umejaa Malaika, kasema, ‘Si lazima utoke msalabani, elekeza tu kidole Chako, Tutabadilisha hali ya mambo.’”

110 Lakini akasema, “Mimi sikuzote hufanya yale yanayompendeza Baba.” Ati nini? Chanjo ilishikilia. Neno na mapenzi ya Mungu yalikaa ndani Yake, haidhuru kama alipigwapigwa mgongoni na kuitwa Rabi kijana wa Galilaya, ama kama aliitwa Beelzebuli, ibilisi, mpiga ramli, vyovyote vile, makufuru waliyosema juu Yake, ile chanjo ilishikilia. Ndipo wakaangalia jinsi alivyokuwa . . . kama angepiga mayowe na kughairi yote msalabani, lakini ilishikilia. Amina. Kila kitu kilimwacha: kanisa Lake, watu Wake, na hata Mungu alimwacha, kila kitu, lakini ile chanjo ilishikilia.

Miongoni mwa miamba inayopasuka na anga inayoingia giza
Mwokozi wangu aliinamisha kichwa Chake akafa;
Pazia lililofunguliwa lilifunua njia
Ya kwenda kwenye furaha ya Mbinguni na siku isiyo na mwisho.

111 Hiyo ndiyo njia, kurudi kupitia huko. Ilishikilia, haidhuru nini kilichokuja, ama kilichoenda, ilishikilia vivyo hivyo. Chanjo ilishikilia. Walimtazama akifa, sio kama mwoga, kama Mtawala. Yeye kamwe hakutikisika, alilichukua kama Mtawala. Alijua

jinsi ya kufanya hivyo, kwa maana alitiwa chanjo na Roho Mtakatifu.

112 Ndipo asubuhi ya Pasaka, ilithibitisha ilichokuwa. Chanjo ilishikilia, kwa maana Yeye alifufuka katika wafu. Akasema, "Liharibuni hekalu hili, nitalisimamisha siku ya tatu." Haleluya! Alikuwa akifanya nini? Akilinukuu tena Neno la Mungu ambalo Mungu alinena kupitia kwa Daudi tena, baba Yake duniani. Kasema, "Sitamwacha Mtakatifu Wangu, aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi Yake kuzimu." Naye alijua katika saa sabini na mbili uharibifu huingia, kwa hiyo Yeye akasema, "Liharibuni hekalu hili, nitaliinua tena." Kwa nini? Neno la Mungu lilisema kwamba angelifanya. Hivi Roho Mtakatifu yeye yule hakusema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio"? Tutaliepukaje kamwe? Ni . . . Unaye, endapo umechanjwa.

113 Alimwambia yule mwanamke, "Je, waweza kukinywea kikombe ninachokinywea Mimi? Je, unaweza kuchanjwa na chanjo ninayochanjwa nayo? Siwezi kukupa mkono wa kuume na wa kushoto kwa ajili ya wanao, lakini kama unaweza kukinywea kikombe hiki, na kufanya jambo hili, itakuwa sawa." Bila shaka. "Si kwangu Mimi kutoa hilo, bali wewe kinywee kikombe ninyweacho, chanjwa na Roho yeye yule niliyebatiziwa, na kila kitu kitakuwa sawa."

114 Wakati hao wanafunzi waliposimama pale kwenye Pasaka, kundi la maskini wanawake pale kaburini, nao walikuwa wamegundua kwamba . . . Mariamu alianza kuondoka, akilia, alikuwa na huzuni, ndipo akasikia mtu akiliita jina lake, akatazama huku na huku, akaona ilikuwa ni Yeye, hakuwa amekufa, alikuwa amefufuka tena.

115 Kasema, "Enendeni, mkawaambie wanafunzi Wangu nitakutana nao huko Galilaya. Nimerudi, lile nililosema hasa, chanjo ilishikilia. Nilikufa kama vile Biblia ilivyosema ningekufa, Nafsi yangu ikashuka kuzimu kama Biblia ilivyosema ilifanya, nami ninazo funguo za mauti na kuzimu. Nimefufuka . . . nimefufuka tena, nami ni hai hata milele." Ushahidi, thibitisho lake, chanjo ilishikilia. Amina. Loo, jamani!

Wanafunzi hao walipoona hilo, walisema, "Tunataka chanjo hiyo pia, tunataka hiyo."

116 Akasema, "Pandeni huko juu, kwenye mji wa Yerusalemu, na mngoje huko hata nitakapotuma ile Sumu. Kama mkitaka Uzima wa Milele, kama mkitaka kufanya jambo hili ambalo nimefanya, jambo hili nililo nalo kwa ajili ya ufufuo, mnataka Kitu kitakachowaweka jinsi kilivyoniweka Mimi, mnataka Kitu kitakachowaacha mfe kama nilivyokufa mimi, mnataka kitu Fulani kitakachowafufua kutoka kaburini, nitakirudisha juu yenu. Pandeni moja kwa moja kule juu mkangojee."

117 Sasa, kamwe Yeye hakusema, "Nendeni mkapate. . .digrii yenu ya LL.D." Kamwe hata hakusema, "Enendeni mkajifunze ABC zenu." Alisema, "Ngojeni hata mtakapochanjwa, mtakapovikwa Uweza utokao Juu. Baada ya haya, akiisha kuwajilia Roho Mtakatifu juu yenu, nanyi mtakuwa madaktari Wangu." Amina. Amina. "Ngojeni. Kaeni huko juu na mngojee." Sio, "Nendeni miaka minne katika seminari, na upuuzi huu mwingine wote, na kupata digrii hizi zote, na kushindiliwa dawa hii ya kufanya mwili usioze." Wewe si nungubandia, wewe ni mwana. "Ngojeni mpaka mtakapovikwa Uweza, mpaka chanjo ya Uzima wa Milele iwajilie juu yenu, nami nitawafufua siku ya mwisho, tena."

118 Jamani, alipata baadhi ya wataradhiwa mara moja. Nilipoisikia kwa mara ya kwanza nilikuwa mmoja pia, sikujali walichoniambia, nilitaka Hiyo. Na sikuzote nilisema, "Kama *Hili* si *Lile*, ninataka kuweka *Hili* mpaka *Lile* litakapokuja." Naam. Hiyo ndiyo niliyotaka, chanjo hiyo.

119 Wakapanda huko na kungoja siku kumi. Loo, jamani! Loo, wakati kwa ghafla, wakati Chanjo iliposhuka kutoka Mbinguni, kama upepo wa nguvu ukienda kasi, nayo ikamjaza kila mmoja wao, ikawachanja mia moja na ishirini. Loo, ulikuwa ni wakati wa jinsi gani! Hiyo ilikuwa ndiyo njia ya kurudi. Loo, jamani! Wote walijazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha zingine, Ndimi za Moto zikiwakalia juu yao, Mungu, ile Nguzo kuu ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli, Mungu.

120 Si Miungu watatu: Mungu mmoja, Mungu mmoja. Si Miungu watatu, bali Mungu mmoja katika ofisi tatu, aitwaye Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Baba Mungu katika Nguzo ya Moto, Mungu Mwana katika Mwanawe Mwenyewe, Mungu Roho Mtakatifu ndani yako, Mungu yeye yule akijishusha, akishuka, akiifanya njia Yake kuingia ndani ya mioyo ya wanadamu. Naam, bwana.

121 Hapo waliona ushahidi wake, ahadi ya Yesu. Hapo waliona Nguzo hii ya Moto ikianguka miongoni mwao na kujitenga Yenyewe, nazo Ndimi za Moto, Ndimi za Moto zilizogawanyika zikakaa juu ya kila mmoja wao, Nguzo ile ile ya Moto iliyokuja pamoja na Israeli kupitia jangwani.

122 Hapo Mungu alikuwa akijigawanya Mwenyewe miongoni mwa Kanisa Lake. Kama vile mwanamume na mke wake walivyo mmoja, vivyo hivyo Mungu na Kanisa Lake ni Mmoja, kuna Mmoja. "Siku hiyo mtajua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Mimi ndani yenu na ninyi ndani Yangu." Hiyo ndiyo chanjo; hiyo ndiyo chanjo aliyokuwa nayo, hiyo ndiyo chanjo aliyoipokea. "Si Mimi nizitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu akaaye ndani Yangu, Yeye huzitenda kazi hizo." Sio mimi niyaonaye maono haya, ni Baba yangu, siwezi kufanya lolote.

"Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile *amwonalo* Baba analitenda, ndilo Mwana alitendalo vile vile."

123 Hiyo ndiyo chanjo kutoka kwa kutokuamini, inakutia nanga katika imani iliyo imara ya Kristo, inakutia nanga. Hapo unajua ya kuwa umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, hakuna mtu anayeweza kukuzungumzia utoke kwake, hakuna mtu anayeweza kulielezea likuondokee, ulikuwa kwenye mchanga huo mtakatifu pamoja na Mungu pekee, nawe unajua ulizaliwa mara ya pili, maisha yako yote yamebadilishwa nawe ni kiumbe kipya, hakuna pepo wa kutosha kuzimu wanaoweza kuiondoa kutoka kwako. Wewe ni kiumbe kipya, uumbaji mpya. Umechanjwa kwa nguvu za Mungu, Sumu ya Roho Mtakatifu wa Mungu imekuvutia. Amina.

124 Unajua, Yeye ni Ninyoro ya Bondeni. Kasumba hutoka kwa ninyoro tunajua hilo. Loo, jinsi ilivyo, wakati hao waota ndoto za mchana wanapopata kasumba, wanafikiri hicho ni kitu fulani. Loo, wanapaswa kupata chanjo ya Hii mara moja! Dozi moja kwa wakati wote. Si ndoto ya mchana, bali ni uhalisi wa Mbinguni, uliotiwa nanga ndani ya nafsi yako kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Inakufanya ulale, si usingizi, bali umekufa kwa mambo ya ulimwengu na u hai ndani ya Kristo, ambaye ni Kristo yeye yule anayeishi milele na milele. Inakufanyia kitu ambacho hakuna anayejua ila wewe. Wewe ndiye uliyekunywa hiyo Dawa ya chanjo, wewe ndiye uliyepata hiyo chanjo, unajua inahusu nini. Kwa nini? Uliihisi, uliijua, uliona kile ilichokufanyia, ilikufanyia jambo fulani, umetiwa alama. Amina. Unajua mahali ulipo.

125 Tulikuwa tunatia ndama alama. Kulikuwa na mwanamke aliyejitokeza, wakati mmoja, akiwa juu ya farasi, naye akasema, "Je, hivi hamwoni aibu kufanya hivyo, maskini jamaa huyo mdogo, mkimwekea alama hiyo juu yake?"

Nikasema, "Inauma kwa muda kidogo, lakini anajua yeye ni wa wapi." Amina. Ndivyo ilivyo.

126 Mungu anakufanya uumie kwa muda kidogo, lakini unajua wewe ni wa wapi baada ya hayo. Anapomimina chanjo Yake ya Chuma cha kupiga chapa cha Roho Mtakatifu juu ya mwanamume au mwanamke, anambadilisha kutoka kile alichokuwa hadi kile alicho. Anajua ni wa malisho gani, haruhusu haramia yeyote amwongoze. Ana Makao, ana malisho, ana makwao, naye Roho Mtakatifu ndiye yule Kiongozi, Yule anayemwongoza kwenye maji matulivu na kumpa Uzima wa Milele.

127 Walipowaona watu hawa wakipoteza kiburi chao chote, walianza kucheza katika Roho, wakafikia kunena kwa lugha, Ndimi za Moto zilizogawanyika zikiruka kutoka kwao, nao hawa hapa wote wanatoka, kundi la Wagalilaya wakinena katika kila lugha chini ya Mbingu, hawakujua yote haya yalimaanisha

nini, madaktari hao wa uungu walishangaa sana, hawakujua kilichokuwa kimetukia, lakini walikuwa wamechanjwa, mnajua, wakaanza kuulizana, haya yote yanamaanisha nini. Hayo maswali yalipoibuka: "Je, kumesalia Zeri yoyote Gileadi? Kuna Tabibu yeyote huko?" walikuwa na Tabibu, walikuwa na Tabibu Mkuu, walikuwa na tabibu wa duniani, mnajua jina lake lilikuwa nani? Dk. Simoni Petro, akajichukulia kisanduku kidogo cha sabuni, akasimama juu yake, kisha akawatolea hotuba.

Wakasema, "Sisi ni wataradhia wa hilo. Tutendeje tupate kuokoka?"

"Je, mnataka jambo hili, ndugu?"

"Naam."

128 "Mbona, Hili, nitawaambia huko nyuma katika Maandiko linakotoka." Daktari yeyote mzuri hurudi kwenye fomula yake. Ah, loo, loo! Rudini nyuma! "*Hili* ndilo *Lile* lililonenwa na nabii Yoeli, 'Basi itakuwa katika siku za mwisho,' asema Mungu, 'nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili.'"

Wakasema, "Petro, Dk. Simoni Petro, tufanye nini tupate kuokoka?"

129 Akasema, "Nitawaandikia maagizo, wala hayatakuwa yanayoweza kubadilishwa, ni maagizo ya Milele." Kasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana agizo hili ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Hayo ndiyo maagizo. Loo, ndugu! Yafuateni tu. Kuna Zeri nyingi iliyobaki katika—katika Gileadi, na tuna matabibu wengi hapa. Hiyo ni kweli.

130 Mnajua nini? Kama daktari akiandika fomula, naye mtaalamu wa dawa tapeli akaipata, naye aweke kiuasumu kingi kupita kiasi au kisichotosha, atamwua mgonjwa wako. Hiyo ndiyo imekuwa shida siku hizi, maagizo yameandikwa, maagizo hayo ya Milele katika siku ya Pentekoste, wataalamu tapeli wengi kupita kiasi wa dawa, wanaojiita madaktari, wameingiza vitu vingine ndani yake, nao wameliua kanisa, mpaka kundi la wanawake waliokata nywele, wanaovaa kaptura . . . Hiyo ndiyo shida, hiyo ndiyo sababu wanawake wetu wananyoa nywele zao, nao wanaume wetu wanaunda madhehebu, na kadhalika, bila ujasiri wa kutosha wa kujitokeza, hawajatekeleza lile agizo kikamilifu.

131 Unataka kujua njia ya kurudi? Hiyo ndiyo, hivyo ndivyo Petro alivyosema, Dk. Petro, yule anayetoa chanjo. Kristo aliijaribu Mwenyewe na ikafanya kazi, Petro alikuwa nayo, nayo ikafanya kazi, ninayo, nayo inafanya vizuri sana. Hayo ndiyo maagizo, usijaribu kuyachezea, usijaribu kuongeza kitu kwake. Ukiweka sumu nyingi kupita kiasi, utamwua mgonjwa wa—

wako, bila shaka kabisa, daktari alijua jinsi ya kusawazisha maagizo hayo. Hiyo ni kweli.

132 Kwa hiyo, ukitaka kujua jinsi maagizo yanavyotolewa, Yeye ameyaandika papa hapa katika Matendo. Hiyo ndiyo njia ya kuifanya. Hasa. Sio, "nenda ukapeane mikono na mhubiri, na kunyunyiziwa matone machache ya maji juu yako," na *kitu kingine*. Yeye alitoa hayo maagizo papa *Hapa*, nawe uyatekeleze kikamilifu, ndipo matokeo yale yale yatakuja, hiyo ni kweli kabisa, maana Yeye kamwe hakuyajaribu kwa nungubandia, Yeye aliyajaribu kwa nafsi Yake. Naye Mungu alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu, na kila mwana wa Mungu aliyezaliwa na Roho wa Mungu, "Ni kwa ajili yako, na kwa watoto wako, kwa wote walio mbali, wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie, maagizo haya yatafanya kazi." Amina! Sina kichaa, lakini nimechanjwa, amina, Kitu fulani kinateremka *humu* ndani. Najua ni kweli, nimeijaribu, najua ni kweli.

133 Matokeo yale yale waliyokuwa nayo: "Ishara hizi zitafuatana na hao, aminini. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu. Nia iliyokuwa ndani ya Kristo na iwe ndani yenu," kama nia iyo hiyo iko mle ndani pamoja na nguvu zile zile zilizo mle ndani, utafanya kazi zile zile alizofanya Yeye.

134 Ukiondoa sumu yote ndani yake, na madhara yote, mtu fulani, aseme, "Naogopa kusema..." Dondoadume wewe. Mungu anataka wanaume. "Sipendi kusema..." Loo, wengine wanahitaji kuwa na, sijui nini. Wanahitaji chanjo. Naam, bwana. Tunachohitaji, chanjo. Naam, bwana. "Ni kwa ajili yenu na watoto wenu, wale walio mbali."

135 Sasa, kama wewe, unaona, ukiweka sumu nyingi kupita kiasi ndani yake, unamwua mgonjwa wako. Hiyo ni kweli. Hutaki kuwa mjuvi, na fidhuli, na dhalimu, na mkandamizaji, unaona, kwa kweli uliyopata; hapo ndipo ninyi ndugu wa Umoja mlipokosea. Sasa, tunarudi barabarani, tunarudi kwenye tiba. Na ninyi ndugu wa Assemblies mliojitenga, kila mmoja wenu, hapo ndipo mlipokosea. Ukweli unapoongezwa, endelea tu, achana nao, Mungu ataushughulikia. Hakuna mtu anayeweza kuja Kwake isipokuwa Yeye amwite kwa vyovyote vile. Kweli.

136 Njia ya kurudi, ndugu, ni ushirika na ndugu wote. Hiyo ni kweli. Kuchanjwa kutokana na chuki, kuchanjwa kutokana na kijicho, kisha kuchanjwa kutokana na mambo ya ulimwengu, kurudi kwenye chanjo ya Roho Mtakatifu kwa nguvu zilizomfufua Yesu kutoka kaburini na kulitia Kanisa moto kwenye siku ya Pentekoste, kurudi kwenye chanjo hiyo.

137 Haya hapa maagizo: "Haya hapa maji; ni nini kinachokuzuia?" Huyu hapa Roho kote katika kanisa; kuna shida gani? Mungu atauliza "Kwa nini?" siku moja. Hakika. Ukiondoa maagizo yako yote, na kuogopa kusema lolote kwa

kanisa lako, na kuogopa dhehebu lako litakufukuza, unafanya nini? Hata afadhali uwape maji ya kunywa, hayana dawa ndani yake hata kidogo. Hiyo ndiyo sababu wanafanya jinsi wanavyofanya. Hiyo ni kweli. Unahitaji maagizo, hiyo ndiyo njia ya kurudi, hivyo ndivyo ilivyoanza, hivyo ndivyo Mungu alivyolianzisha Kanisa Lake. Basi unapotoka kwenye barabara hiyo, umetoka barabarani. Wakati tulipounda madhehebu, na kupeana mikono, na kuchukua kunyunyiziwa badala ya ubatizo, na tukakubali kupeana mikono badala ya Roho Mtakatifu, au kutia mkate mwembamba kinywani mwako badala ya Roho Mtakatifu, ulitoka barabarani.

138 Kasisi wa jeshi siku moja alisema, wakati mtu mmoja alipopigwa risasi kwa bomubomu, alisema, "Kapteni, unamjua Mungu?"

Akasema, "Wakati mmoja nilimjua."

Kasema, "Uli—ulimjua lini?"

Akasema, "Siwezi kukumbuka."

Kasema, "Ulimwacha wapi? Itakubidi kurudi pale ulipomwacha kusudi umpate."

Akasema, "Sijui."

Akasema, "Mapafu yako yanajaa, bwana, afadhali ufikirie kwa utulivu na haraka."

Kwa hiyo, akalala pale kidogo, naye akasema amani kuu ilikuja usoni mwake, kasema, "Nakumbuka. Nakumbuka pale nilipomwachia."

Akasema, "Ilikuwa wapi?" Akasema, "Anzia papo hapo."

Akasema:

> Sasa najilaza chini kupata usingizi,
> Namwomba Bwana nafsi yangu ailinde;
> Kama nikifa kabla sijaamka,
> Namwomba Bwana nafsi yangu aichukue.

Akavuta pumzi yake ya mwisho huku mabubujiko ya damu yakiyajaza mapafu yake kisha akafa. Alifanya nini? Alimpata Yesu pale pale alipomwacha.

139 Hapo ndipo Kanisa litakapompata. Kamwe hutampata katika dhehebu; Yeye hayuko huko. Kamwe hutampata katika namna fulani ya mipango ya elimu; Yeye hayuko huko. Utampata katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, na hapo ndipo mahali pekee utakapompata. Amina.

140 Huu ndio ukweli, ndugu. Kurudi, hii ndiyo njia ya kurudi. Usiyachezee hayo maagizo, yachukue, yaamini, ujazwe na Roho Mtakatifu, ni kwa ajili ya kila kizazi. Angalieni, "Ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Kila mtu, agizo hili ni kwake, si kupeana mkono ama chochote kile, bali

lile agizo, jinsi hasa Petro alivyoyanena *Hapa* na kuyaandika, naye Mungu akayaandika kwa Roho Mtakatifu katika Matendo 2:38, ni kutubu kila mmoja wenu, sio kusema tu, "Naam, ati tubu? Sasa, vema, ninapanda niende nikajiunge na kanisa." Hiyo haimaanishi hivyo. "Vema, nitapanda niende nikabatizwe, na hilo latosha." La bwana, maji hayakuokoi. Tubu la sivyo uangamie. Si ubatizo ili kuzaliwa upya, najua baadhi yenu mnaamini hilo, lakini mnawezaje kuchukua hilo? La, bwana. Tubuni! Maagizo yalisema toba ndiyo inayotangulia, kisha mbatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu. Ukiisha kutubu basi wewe ni mtaradhia wa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nayo ahadi hii ni kwa ajili yenu, na watoto wenu, kwa wote walio mbali.

141 Loo, ninyi Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wanazarayo, Pilgrim Holiness, Wakatoliki, Wapentekoste, kuna nini? Kuna nini? Mungu atakaposhuka kunena katika nguvu na utukufu Wake, ndipo mtashangaa yote yanahusu nini. Hiyo ndiyo sababu mna kanuni hizi za imani na kadhalika, na kuingiza mafundisho haya ya sharti na kadhalika, mpaka imeenda mbali kabisa. Enyi watoto, rudini, hiyo ndiyo njia ya kurudi, yachukueni hayo maagizo. Ondoleeni mbali ugonjwa huu wa dhambi, kutokuamini huku. Mrudieni Mungu, aminini kwa moyo wenu wote. Na tuombe.

142 Ninakuamini, Bwana, ninakuja pamoja na kanisa hili usiku wa leo, ninaamini, Bwana, pamoja na watu wanyofu sana kadiri niliowahi kukutana nao. Ninaomba, Bwana, kwamba hawatafikiri kwamba tunasema mambo haya ndani yetu wenyewe, jalia wapate kujua kwamba ni mzigo, uchungu moyoni kulazimika kusema mambo haya, lakini hata hivyo, tabibu wa kweli atakuwa mwaminifu kwa maagizo yake. Bwana, jalia yajazwe katika kila moyo usiku wa leo.

143 Ikiwa watu humu ndani wamepokea tu ubatizo wa Yohana, kama vile Paulo alivyowapata, na watambue kwamba kuna ubatizo mwingine, kwamba kuna ubatizo wa Roho Mtakatifu; ikiwa kitu pekee wajuacho ni kupeana mkono na mhudumu, au kujiunga na kanuni ya imani, na wajazwe na Roho Wako Mtakatifu. Tujalie, Bwana. Na waje kwa unyenyekevu, na wapate majaliwa haya, na warudi kwenye Barabara ya Azusa tena, waje moja kwa moja hadi kwenye Pentekoste tena, kwa Ufalme na utukufu wa Mungu. Ninawakabidhi Kwako mbele ya Madhabahu Yako ya dhahabu, mahali ilipo Dhabihu yetu, Yesu Kristo. Utupokee, Baba.

144 Wewe ni Mungu, Daima ulikuwa Mungu, daima utakuwa Mungu, Maneno Yako hayawezi kushindwa. Uliposimama hapa, ukifanyika mwili duniani katika Mwana Wako Mwenyewe, Maskani uliyoijenga upate kukaa ndani yake, jinsi hiyo inavyowapofusha watu! Naam, je, seremala hajijengei nyumba

ya kuishi? Je, Mungu, yule Mjenzi mkuu, hakujijengea Mwenyewe Nyumba ya kuishi?

145 Ee Mungu, jalia waone kwamba si nyumba, ni kile kilicho ndani ya hiyo nyumba, Mjenzi wa hiyo nyumba. Na jalia watambue ya kwamba huyu Roho Mtakatifu, kupitia kwa kifo, kuzikwa, na kufufuka kwa nyumba hiyo ambayo Mungu aliishi ndani yake, kupitia hiyo Damu isiyoghoshiwa ya Uumbaji Wake Mwenyewe, alisafisha njia ili Mungu apate kukaa ndani ya mioyo yetu sisi wenye dhambi, kwa neema.

146 Sasa unaiendeleza kazi Yako kupitia Kanisa Lako, kupitia chombo cha mwanadamu, ambacho daima kimekuwa ndiyo njia Yako ya kufanya hivyo. Mungu, jalia wanaume na wanawake hapa usiku wa leo, chini mioyoni mwao, wapate njaa na kiu; tuko katika wakati wa yubile, tunaadhimisha, Bwana, juma hili la yubile ya neema na utakatifu Wako mkuu uliyoimwaga juu ya Kanisa Lako miaka hamsini iliyopita, hapa katika jimbo hili.

147 Na Baba Mungu, huu ni wakati wa yubile, nao watu wanajua jinsi ya kurudi, ni jinsi walivyoanza kutoka mara ya kwanza. Rudini kwa Roho Mtakatifu, rudini mkayakatae mafundisho haya ya sharti ambayo madhehebu yameingiza ndani yake, rudini mkaponywe kwa nguvu za Mungu. Tujalie, Baba.

148 Sasa, tunajua kwamba mambo haya yote yamefanya kazi kwa manufaa kama ahadi Yako, maana Wewe uliionyesha kama mfano katika Israeli, kama tulivyokuwa nalo jana usiku. Sasa jalia Mungu wa—wa Yesu Kristo, jalia Yeye aliyekuwa Imanueli, jalia Yeye aliyesimama duniani hapa na kusema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya," na lifanyike, Bwana. Tunaikabidhi ibada, maneno, samehe njia isiyo na ufasaha yanayotolewa kwayo, Bwana, lakini ninaomba ya kwamba utayazamisha katika kila moyo, nayo yataleta kanisa takatifu lililojazwa na Roho, kurudi kwenye siku ya Pentekoste tena, katika Jina la Yesu, ninakupa Wewe. Amina.

149 Mnaamini? Nataka usikivu wenu mkamilifu kwa muda mfupi tu. Nawatakeni mwamini kwa moyo wenu wote. Biblia inasema, Bwana Mungu ametuahidi kwamba wote walioamini waliokolewa. Sasa, hilo linasikika dogo sana, lakini unaona, unapoamini kweli, hilo ndilo tu unaloweza kufanya. Ndipo Mungu hana budi, unapoamini kweli, ndipo Mungu anakumwagia Roho Mtakatifu, na kisha Mungu analithibitisha Neno Lake. Sasa, Biblia ilisema . . .

150 Ngoja kidogo, naamini, kabla sijafanya hili, ninaamini kulikuwa kuwe na mstari wa maombi. Hiyo ni kweli? Vema. Ni wangapi wanataka kurudi kwenye Pentekoste? Inueni mikono yenu. Ni wangapi wanaoamini kwamba yale maagizo yangali yanatumika? Amina. Ni ya hakika. Ubatizo wa Roho Mtakatifu, sio elimu, sio kupanda kwenda kupata Ph.D. yako na halafu . . .

151 Nikodemo alipokuja kwa Bwana Yesu—Yesu, akasema, "Nifanye nini nipate Uzima wa Milele?" mtu, mwenye umri wa miaka themanini, amekuwa kuhani maishani mwake mwote. "Nifanye nini nipate Uzima wa Milele?"

152 Yesu hakusema, "Nenda ukaiboreshe elimu yako." La. Hakusema, "Nenda ukatafute ofisi ya juu zaidi katika shirika lako." La. Alimwambia waziwazi, Yeye—Yeye—Yeye alimkemea kabisa kwa kuwa mtu wa hadhi yake, halafu asiyajue mambo hayo, ya kwamba huna budi kuzaliwa mara ya pili. Hakika.

153 Ni jambo lile lile usiku wa leo. Mnaona, tunalichukulia kirahisi mno. Tunachukua tu aina fulani ya mhemuko, unasema, "Nilizaliwa mara ya pili," na kuendelea, nayo maisha yako yanathibitisha kuwa hayafanyi hivyo? Kuna kasoro fulani. Naam, bwana.

Loo, unasema, "Lakini najua mtu huyo ni mtu mzuri." Haijalishi yeye ni mzuri kiasi gani, hilo halina uhusiano wowote nalo.

154 Hukutani na watu wazuri kuliko Waislamu, na mambo kama hayo, wazuri na kila kitu, la hasha, loo la, wakati mwingine makafiri, waabudu sanamu, wazuri na wanyenyekevu wawezavyo kuwa, hilo halimaanishi chochote. La, bwana.

155 "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hivyo ndivyo Daktari alivyosema, haya ndiyo matokeo ya chanjo, haya basi. Naam, bwana. Jambo ndilo hilo. Daktari alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Je, alisema hivyo? Hiyo ndiyo ishara ya mwaminio. Tunachukua ishara kuwa ni mtu mwema, anaenda kanisani na kutoa zaka zake. Hilo ni jema, ni sawa, lakini hivyo sivyo Yesu alivyosema: "Ishara hizi zitafuatana na hao; kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya." Maana kama uhai ulio katika mpichi unaweza kutolewa kwa mpichi, na kuingizwa kwenye mtofaa, hautazaa matofaa tena, bali mapichi, kwa sababu chembe ya uhai hai wa mpichi iko kwenye huo mtofaa, nao hauna budi kuzaa mapichi. Hiyo ni kweli kabisa.

156 Ndugu Williams ameketi hapa mbele yangu, rafiki yangu msiri, mwema sana. Mimi...alimpigia simu Ndugu Sharrit asubuhi ya leo, nami nikamwombea kwa simu. Nilikuwa nimesimama na Ndugu Sharrit siku moja kwenye shamba la michungwa, na kulikuwa na mti umesimama pale, m—mti wa, naamini ulikuwa mchungwa, nao ulikuwa na—ulikuwa na aina nne au tano za matunda juu yake. Nami nikasema, "Mbona, huo ni mti wa aina gani, Ndugu John?"

Akasema, "Ni—ni mchungwa."

"Vema," nikasema, "Ninaona balungi, chenza, kangaja, ndimu, matunda haya yote mbalimbali."

Akasema, "Loo, naam."

Nikasema, “Vipi?”

Akasema, “Yamepandikizwa.”

“Vema,” nikasema, “sasa, hiyo ni ajabu, sivyo?”

Akasema, “Naam, chochote kilicho na uhai wa mchungwa kitaishi nao.”

Kasema, “Hilo ni jema sana.” Nikasimama, Kitu fulani kikanisimamisha, nikaangalia tena.

157 Kama siku ile, kule Ufini, wakati yule mvulana mdogo alipokuwa amelala maiti; nikasema, “Ndugu Moore, huyo ni yule jamaa mdogo niliyekwambia habari zake papa hapa Shreveport, mvulana mdogo angefufuliwa katika wafu mahali *fulani*, huyo—huyo ndiye, hana budi kurudi, mauti haiwezi kumshikilia tena, Mungu alinena.” Nikasema, “Ewe mauti, mwachilie.” Huyu hapa. Amina. Mungu hawezi kusema uongo. La, la. Mnaona?

158 Nikasema, “Ndugu John, ninaona jambo fulani. Unaona,” nikasema, “sasa, nataka kukuuliza jambo fulani, Ndugu John, maana ninataka kuchukua mahubiri kutokana na jambo hili.” Nikasema, “Sasa, mwaka ujao hayo, matunda hayo yote aina ya chungwa, kama ndimu, na chenza, na balungi, hayo yote yataanguka, nayo yatazaa machungwa?”

159 Akasema, “Loo, la, la, la, la,” akasema, “litazaa kwa jinsi yake.” Akasema, “Lile lililo na tawi la limau ndani yake litazaa limau, nalo linalozaa, lililo na che—che—chenza litazaa chenza.”

“Mbona,” nikasema, “nilidhani ulisema ni mchungwa!”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Kwani uliacha kuzaa machungwa?”

Akasema, “La, wakati huo mti wa asili utakapotoa tawi la asili, huzaa chungwa.”

160 Ndivyo hivyo. Ndivyo hivyo. Madhehebu haya yamepandikizwa, yangali yanazaa matunda ya kimadhehebu: uanachama, kadhalika. Lakini wakati ule Mti utakapozaa tawi la asili tena, kutakuwa na Kitabu cha Matendo kitakachoandikwa nyuma yake.

161 “Mimi ni Mzabibu, ninyi ni matawi.” Kwa nini? Maisha yaliyo—yaliyoingizwa kutoka kwa Mzabibu wa asili yakizaa tawi, ni tawi la Kipentekoste lenye matokeo ya Kipentekoste, kwa maana Uzima wa Kristo uko ndani ya hilo tawi, nalo linafanya kazi Zake. Hmm!

162 Si—sina karama ya kunena kwa lugha, lakini hakika ninajisikia kama ningetaka. Loo, jinsi Roho anavyoshuhudia nafsini mwangu! Anashuhudia pamoja na Neno kwamba mambo haya ni kweli.

163 Mnaamini? Ni wangapi wenu hapa ndani walio na kadi za maombi, inua mkono wako. Sasa, wekeni mikono yenu chini. Ni wangapi hapa ndani wasio na kadi za maombi, na hata hivyo

wewe ni mgonjwa, unataka kitu kutoka kwa Mungu, inueni mikono yenu. Vema, aminini.

164 Baba yetu wa Mbinguni, najua ninasimama mbele ya kusanyiko ambalo, wengi kiasi ni wageni, namhisi Roho Wako akitulia sasa. Nimenena Neno Lako na kusoma maagizo Yako; nimewaambia watu hiyo ndiyo njia ya kurudi.

165 Sasa, Nikodemo alitambua, na vivyo hivyo Baraza la Wazee, wakati walipokuona Wewe ukiwa umefanyika mwili, walisema, "Rabi, tunajua Wewe ni Mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, kwa maana hakuna mtu angeweza kufanya mambo haya unayofanya Wewe isipokuwa Mungu awe pamoja naye." Nalo kundi lilo hilo, likijua hayo kwa kazi alizosema alizifanya Yeye, na akaahidi kwamba waaminio Wake watafanya kazi ile ile, walimwita Beelzebuli, na wakasema Mafundisho Yake yaliwadanganya watu.

166 Wakati haujabadilika, Baba. Tuko kwenye zao lingine, lakini Wewe ulidumu moja kwa moja, kutokuamini hakukukuzuia, ulisonga mbele vivyo hivyo, ukifanya yale ambayo Baba alikwambia ufanye, ulipotoa tamshi Lako wazi, kasema, "Sifanyi chochote, Mwana hawezi kutenda chochote kwa nafsi Yake Mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda."

167 Uliweza kumwambia Filipo mahali alipokuwa chini ya mti wakati Nathanaeli alipompata; uliweza kumwambia Simoni kwamba alikuwa mwana wa Yona, ukalitaja jina lake na jina la baba yake; ulimwambia yule mwanamke kisimani; Wewe . . . imani ya mtu mmoja kipofu ilikusimamisha; maskini mwanamke mmoja aliyetokwa na damu aligusa upindo wa vazi Lako, haiwezekani kabisa Kwako kuuhisi kimwili, lakini ulisimama na kumwambia shida zake, kisha ukasema zilikuwa zimekwisha.

168 Jalia ule Uzima uliokuwamo ndani ya Kristo uje katika kundi hili kwa dakika chache tu, Bwana, wapate kujua ya kuwa Wewe ungali ni Mungu. Nimemalizia tu kuwaambia hivi punde, Bwana, Neno Lako. Watu wakija huku na kusema *hili*, *lile*, na kila vitimbi vidogo; lakini Bwana, inashuhudia nini? Kuna Mmoja wa kweli mahali fulani. Bwana Mungu, jalia atokee usiku wa leo, jalia Roho Mtakatifu anene wala si mwanadamu.

169 Lipe imani kanisa hili, Bwana. Ninatambua usingeweza tu kumtia mafuta mmoja wetu, huna budi kuwatia mafuta wengi wetu. Ututie mafuta pamoja, Bwana, kama Kanisa Lako, na ijulikane ya kuwa Wewe ni Mungu, nami nimesema kweli. Ninasimama juu ya Neno Lako, hata kupitia upinzani, lakini nimejaribu kuwa mkweli; sisemi hilo kwa ajili yangu mwenyewe, Bwana, wala si kwa ajili ya watu hawa wanaonisikia, lakini ninaomba kwa sababu shindano la kuamua limekaribia. Ninaomba ya kwamba utalithibitisha Neno Lako usiku wa leo, Bwana, ya kwamba ni Kweli, ya kwamba Uhai uliokuwa

ndani ya Kristo unaishi katika Kanisa Lake na waaminio Wake. Tujalie, Baba, kupitia kwa Jina la Yesu Kristo. Amina.

170 Ninataka kila mtu awe na kicho uwezavyo. Ni wangapi humu ndani ambao ni wageni kwangu? Inueni mikono yenu. Ningeweza tu kulihisi; hamjawahi kuwa mikutanoni hapo awali.

171 Sasa, Yesu Kristo alisema katika Neno Lake katika Yohana Mtakatifu, 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Je, mnaamini hilo? Biblia ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Mnaamini hilo? Waebrania 13:8. Vema. Vema.

172 Sasa, njia pekee ya kujua kama ni Kristo au la, si mavazi, maana Yeye alivalia kama watu wa kawaida, kama angalikuwa hapa usiku wa leo angevaa suti kama tuliyovaa, haikuwa ni vazi Lake, sio kwa sababu alikuwa na ndevu, ama hakuwa na ndevu, ilikuwa ni Uhai uliokuwa ndani Yake ambao ulithibitisha kile alichokuwa. Watu wengi walivaa kama Yeye katika siku hiyo, lakini hawakuwa Yeye. Hiyo ni kweli. Watu wengi siku hizi wanafanya jambo lile lile, lakini halilibadilishi hata kidogo, ni yale maisha. Sasa, jinsi walivyojua ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Kristo ni kwa sababu iliwabidi kufuata vile Maandiko yalivyosema Kristo angekuwa. Je, hiyo ni kweli?

173 Sasa, Musa aliwaambia Kristo angekuwaje? Angekuwa nabii kama yeye. Je, hiyo ni kweli? Nao wote walimtazamia, kwa maana Mungu alikuwa amewaambia, "Akiwako mtu miongoni mwenu aliye wa kiroho au nabii, Mimi Bwana, nitasema naye, na kama ndivyo, itakuwa ni kweli, kama sivyo, basi msimsikie." Hiyo ni yenye mantiki kabisa.

174 Na sasa, wakati Yesu alipofufuka, na alipoanza katika huduma Yake naye Simoni akajitokeza, Petro, alimwambia jina lake lilikuwa Simoni, na kumwambia kwamba jina lake lilikuwa Simoni na jina la baba yake ni Yona. Hiyo ni kweli? Hilo lilimfanya mwaminio.

175 Filipo akaenda akampata, au, Nathanaeli akaenda akampata Filipo chini ya mti, akasema, "Njoo, uone Mtu tuliyempata." Ndipo alipomwambia kile kilichokuwa kikitukia, hakuninii, kidogo lilimfadhaisha. Basi alipofika pale, Yesu alimtazama moja kwa moja na kusema, "Tazama, Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake." Sasa, alikuwa—alikuwa mwalimu, alikuwa mtu aliyejua. Alisema, "Rabi, ulinijua lini Wewe?"

Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona."

Kasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ni Mfalme wa Israeli." Hilo lilitosha. Mnaona?

176 Yule mwanamke kisimani, alipozungumza naye, wengi kote katika Maandiko, walijua ya kwamba alipokuwa anakuja

alikuwa awe Nabii-Mungu, hiyo ilikuwa ndiyo ishara Yake, daima imekuwa, na ingali ndiyo. Basi mnaona, ya kwamba tunapotambua, mwanamke huyu alijitokeza, Yeye akasema, "Mwanamke, nipe maji ninywe," alitaka kufanya mazungumzo naye.

Mwanamke akasema, "Si kawaida kwa Wayahudi kuniomba mimi, mwanamke Msamaria, mambo kama hayo, hatuna uhusiano wowote kati yetu."

Akasema, "Lakini kama ungejua ni Nani uliyekuwa unazungumza naye, ungeniomba Mimi maji unywe."

Akasema, "Kisima ni kirefu, huna kitu cha kuchotea," na kadhalika.

Akasema, "Nenda, kamwite mumeo mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume."

Akasema, "Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, naye huyo unayeishi naye si mume wako, umesema kweli."

Akasema, "Bwana . . ."

Sasa, Mafarisayo walipomwona akifanya hivyo, walisema, "Yeye ni mpiga ramli, Beelzebuli." Mnaona?

177 Lakini yule kahaba, yeye alisema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Tunajua ya kwamba ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya, hiyo itakuwa ndiyo ishara ya Masihi. Tunajua atakapokuja, atatwambia mambo haya."

Akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye."

178 Basi mara moja akakimbilia mjini, na kusema, "Njoni, mwone Mtu, aliyeniambia mambo niliyoyatenda. Je, haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?" Nao watu wa huo mji wakamwamini yule mwanamke, na wakamwamini Kristo. Hiyo ni kweli?

Si ajabu alisema, "Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, msiniamini Mimi."

179 Sasa, si lazima tuwe werevu, si lazima tuwe na elimu, inabidi kuamini. Inatubidi kujinyenyekeza na kujifanya wenyewe tupu ili Mungu ajidhihirishe Mwenyewe kupitia kwetu. Jifanye tupu, jiondoe njiani; adui mkubwa kuliko wote uliye naye ni wewe mwenyewe. Sasa, mnamwamini Mungu. Mnamwamini?

180 Sasa, ikiwa Mungu, Baba yetu, ambaye ni Roho Mtakatifu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo ni Roho Mtakatifu, tunajua hilo, "Mimba yake ni ya Roho Mtakatifu," na kama huyo Roho Mtakatifu anaweza kuingia ndani yako na ndani yangu, na kufanya Maisha yale yale aliyoishi Kristo, pako wapi mahali pako pa shaka? Basi nimewaambia ukweli kuhusu kurudi, kurudi mlikotoka. Mnaamini hilo? Kama atafanya hivyo, sisemi atafanya. Sasa, kumbukeni, watu wanaamini ya kwamba siku hizi zimepita, lakini Yeye aliliahidi katika siku za mwisho.

181 Kila mmoja wetu ana ofisi, hatuna budi kuwa waaminifu kwa ofisi hii. Ni Mungu, ni Neno; Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu. Nalo Neno usiku wa leo liko katika miili yetu kujidhihirisha Lenyewe kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu ndani yetu, linazaa tunda Lake. Bila shaka.

182 Kama nilikwambia roho ya Dillinger ilikuwa ndani yangu, unanitarajia niwe na bunduki; kama nilikwambia roho ya—ya msanii ilikuwa ndani yangu, unanitarajia kuchora picha; nikiwaambia Roho wa Kristo yuko ndani yangu, basi fanya kazi ya Kristo. Ndiyo yale Yeye aliyosema. Je, ingekusaidia kuamini?

183 Hebu niwaambie maskini jambo fulani: Nikizungumza katika Kiwanis mbele ya baadhi ya madaktari mkutanoni hivi majuzi. Nilikuwa nimefanyiwa uchunguzi wa mwili na daktari maarufu, ninaenda ng'ambo, nilifanyiwa uchunguzi wa mwili, nilifanya hivi makusudi. Naye alikuwa akiniruhusu. . . Alinipa GI ya juu na ya chini, na baada ya kuuchunguza moyo, damu, na kila kitu. Mungu ashukuriwe, ulifanywa haraka.

184 Kwa hiyo—kwa hiyo ni—nilipoinywa kemikali hii inayoingizwa tumboni kabla ya kupigwa eksirei, nilikakamaa kwelikweli, naye akalisukuma tumbo langu, yeye, akichungulia kwenye eksirei, akasema, "Ndugu Branham?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Tumbo lako linasikika la kawaida, lakini linaninii. . . hakuna kinachotoka."

Nikasema, "Ati halitoi?" Nami nikasema, "Linapaswa kutoa?"

Akasema, "Naam, bwana." Akasema, "Jamani, sielewi."

Nikasema, "Nifanye nini?"

Akasema, "Fikiria juu ya kitu kizuri sana cha kula."

Nikasema, "Unataka nifanye hivyo kwa sababu gani?" Nilijua alichokuwa anaenda kusema.

Naye akasema, "Mnofu mmoja mkubwa, mtamu."

Nikasema, "Nitapatana kwa sahani moja ya kuchakulo aliyekaangwa na maharagwe ya pinto."

Basi akasema, "Sawa, anza." Nikabadilisha, nikaanza kuwazia.

Akasema, "Huyo anaenda."

Nikasema, "Ni nini kilichosababisha hilo, Dak?"

Akasema, "Maskini waya wa umeme ubongoni mwako ulituma neno tumboni mwako."

Nikasema, "Hiyo ni kweli?"

Kisha nikizungumza, nikasema, "Unakumbuka ule waya mdogo?" Nikasema, "Daktari, ni nini kinachokufanya kuota ndoto? Je, ulio-. . . wewe huota?"

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Ni nini, sehemu yako ambayo inaota?”

Akasema, “Dhamira yako ya ndani.”

Nikasema, “Mwanadamu wa kawaida, hii *hapa* dhamira moja, na hii *hapa* dhamira ya ndani, inabidi ulale usingizi ndipo uweze kuingia kwenye dhamira *hiyo*.”

185 Alikuwa ndiyo kwanza aniambie, kasema, “Nilipata kitu fulani, Ndugu Branham, tena, siwezi kukielezea.” Kasema, “Sio mishipa yako,” akasema, “ni kitu fulani kilicho ndani ya mishipa yako.”

Nikasema, “Nafsi yangu?”

Akasema, “Naam.” Kasema, “Mimi. . .Ndiyo inayokufanya ulicho wewe.”

186 Nami nikasema. . .Nilimwuliza kuhusu maono, hakujua lolote juu yake, basi nikamwambia, nikasema, “Dhamira moja iko *hapa*, nyingine iko *hapa*. Inabidi utoke kwenye dhamira *hii*, uiache ilale, upate kuingia *hapa* ndani. Lakini sehemu fulani yako ilienda mahali fulani, kwa sababu unaweza kukumbuka ndoto na maeneo uliyokuwa katika ndoto zako, umbali wa miaka na miaka.”

Kasema, “Hiyo ni kweli.”

187 Nikasema, “Unaona, hiyo ni kawaida, lakini Mungu anaiweka, kwa baadhi yetu, kwamba dhamira zetu za kwanza na dhamira za ndani ziko pamoja; hatulali, Mungu anaitumia tu kuona mambo yaliyokuwako, na yaliyopo, na yatakayokuja, hayo ni ya kinabii.”

188 Naye akasema, “Bw. Branham, nimesoma vitabu vyako kuhusu uponyaji,” akasema, “Hakika nakubaliana nawe,” kasema, “Nitakwambia,” kasema, “tuna visa dhahiri hapa, naweza kuthibitisha hilo, sayansi.” Ikiwa kuna daktari aliye karibu, anaweza kukwambia hivyo. Akasema, “Hebu mtu awe na ugonjwa wa kufisha, au kifua kikuu, au kidonda, au kitu ambacho ni kibaya sana, tunajua kitamwua, nasi tutamwambia hivyo na,” kasema, “kama akivurugika, ashikwe na wasiwasi, akasirike, na kufadhaika, na kuendelea,” akasema, “mgonjwa huyo atakufa mara moja. Lakini tuseme mgonjwa huyo, kwa kawaida kama yeye ni Mkristo, ama chochote kile, hajali kufa, ni moja tu ya mambo ambayo hatuna budi kufanya, kufa ni sehemu ya kuishi, kwa hivyo yeye anaendelea tu na kukabiliana nao, ‘Nitaishi hadi wakati wangu utakapotimia,’” kasema, “hilo, mtazamo huo, karibu huudumaza ugonjwa huo.” Kasema, “Ataendelea kuishi, zaidi, na zaidi, na zaidi, kabla haujamwua.”

189 Nikasema, “Vema, daktari, acha nimalizie hadithi yangu.” Nikasema, “Weka kibaini uwongo kwenye mkono wako, na usimame, kisha ujaribu uwezavyo kufanya uwongo usikike

kama ukweli, ndipo uangalie sindano hiyo ikienda hasi. Kwa nini? Ni mtetemo kwenye mishipa yako, wewe hukuumbwa upate kusema uwongo, uliumbwa upate kusema ukweli. Uwongo ni kitu cha kutisha sana, mpaka unakatiza mishipa yako. Hukuumbwa ili kuwa na hasira, unapaswa kuwa na amani, kama mtoto, pamoja na Mungu. Unaona? Hupaswi kuwa na wasiwasi, unapaswa kuwa na imani, kutembea pamoja na Mungu. Unaona?" Nami nikasema, "Jambo ndilo hilo."

190 Nikasema, "Sasa, Daktari, kama. . .mtu huyu anayeishi katika dhamira hii ya kwanza anaweza kuchukua mtazamo kwamba 'Kama akifa ameokoka, kwa hiyo inaleta tofauti gani?' itaudumaza huo ugonjwa kwa muda mrefu, itafanya nini kama ikitoka kwenye dhamira hiyo ya kwanza, iingie kwenye ya pili, juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu? Itauondolea ugonjwa huo mbali kabisa."

Daktari huyo akasimama, na kusema, "Ajabu sana," machozi yakatiririka shavuni mwake.

Nikasema, "Daktari, unajua shida ni nini?" Nikasema, "Makanisa yetu hayafundishi hilo."

Akasema, "Bw. Branham hiyo ni kweli."

Nikasema, "Tunahitaji kurudi kwenye Pentekoste."

Akasema, "Mimi ni Mpresbiteri," kasema, "mke wangu ni Mpresbiteri."

Nikasema, "Ulijiunga na chama cha Presbiteri."

Akasema, "Ni karibu hivyo."

Nikasema, "Daktari, Mkristo huzaliwa mara ya pili, huwezi kwenda kujiunga, huna budi kuzaliwa."

Akasema, "Bw. Branham, huo ni ukweli," ndipo machozi yakaanza kutiririka mashavuni mwake. Nitambatiza hivi karibuni sana. Um-hum. Um-hum!

191 Ati nini? Iwapo fadhaa zako zitaushikilia huo huko juu, na dhamira yako moja itaushusha chini, na kuufanya mwili wako ufanye kazi vizuri, itafanyaje ukimruhusu Roho Mtakatifu aingie ndani? Itatenda kila kitu ambacho Kristo aliahidi, unakuwa chombo cha Roho Mtakatifu.

192 Nilipozaliwa, kulikuwa na Nuru iliyoning'inia pale. Mnayo hiyo picha hapa mahali fulani. Huo ni ukweli. Kama mimi, nikifa juu ya jukwaa hili, sayansi imethibitisha kuwa ni kweli. Sasa, kwangu mimi, mimi ni mwanadamu, mimi si kitu, mimi ni ndugu yenu tu, hakuna kitu kwangu, bali Roho Mtakatifu, katika kuchaguliwa tangu asili, alichagua karama tangu zamani, Mungu ameweka Kanisani, si kile ambacho mzee fulani alikiwekea mikono yake, Mungu aliweka Kanisani kwanza mitume, kisha manabii, na kadhalika, Mungu aliwaweka mle ndani, wao ni karama za Kiungu, zilizochaguliwa

na Mungu tangu zamani. Kabla Yeremia, nabii, kupata kuzaliwa, Mungu alisema, “Nilikujua hata kabla hujawa tumboni mwa mama yako, nami nikakuchagua na—nabii kwa mataifa, kabla hujatoka tumboni.” Hiyo ni kweli? Hakuwa na uhusiano wowote nalo, Mungu hufanya hivyo. Yeye angali ni Mungu.

193 Sasa, wewe amini kwa moyo wako wote. Nanyi mlio wagonjwa au mlio na haja na Mungu, semeni tu, “Bwana Mungu, nimeusikia ujumbe huu, ni wa ajabu sana kwangu, nimemsikia mtu huyu akidai kwamba Wewe ni Mungu, na Wewe uko papa hapa katikati ya watu.” Kama sivyo, alisema uwongo, “Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nipo papo hapo katikati yao.” Kwa nini? Yeye yu ndani yako kwa vyovyote vile, na anapojigawanya Mwenyewe miongoni mwenu, inarudi kuwa kitu kimoja tena. Sasa, lazima uwe sehemu ya kitu *hicho* ili kuamini kuwa sehemu *hii* ya kitu hicho inaweza kufanya kazi.

194 Kama akinipa huduma, anaye mtu atakayeiamini, la sivyo kusingekuwa na haja ya kunipa huduma. Hiyo ni kweli. Amini kwa moyo wako wote uone kama Mungu hafanyi hilo jambo.

195 Sasa, siwataki ninyi watu mlio na kadi za maombi, ninawataka ninyi watu ambao hamna kadi za maombi, maana nitaziita kadi za maombi. Nataka mweke hili niani mwenu. Sasa, iweni na kicho kabisa.

196 Kristo, sasa, Kristo angeweza kuponya, maana Yeye aliponya kwa ono wakati Baba alipomwambia. Hiyo ni kweli. Yeye kamwe hakumponya mtu yeyote, ama kufanya mwujiza mmoja, mpaka alipoona ono kwanza. Ni wangapi wanaojua hilo? Yohana Mtakatifu 5:19, Yeye alisema Mwenyewe, Yeye ni Mungu wala hawezi kusema uongo.

197 Lakini mnaona, uponyaji tayari umenunuliwa sasa, Dhabihu imetolewa. Yeye angali anaweza kujitangaza Mwenyewe kwa unabii na kuonyesha ishara Zake, lakini uponyaji, huna budi kumwamini. Kama angalikuwa amesimama hapa usiku wa leo, nawe useme, “Bwana, utaniponya?” Aseme, “Tayari nimekuponya; kwani huamini?” Kwa kuwa, “A*li*jeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tu*li*pona.” Je, mnaelewa hilo? Sasa, liamini uone kama Yeye angali hai.

198 Ni changamoto jinsi gani! Nilipinga hilo mbele ya watu nusu milioni wakisimama dhidi yangu, Bombay, India. Niliipinga mbele ya watu laki mbili na nusu huko Durban, Afrika Kusini, nikamwangalia Mungu akiingia jukwaani, wenyeji wavaao blanketi elfu thelathini wakatupa chini sanamu zao na kuwa Wakristo dakika iyo hiyo, nao wanawake, wakiwa uchi wa mnyama, mara Kristo alipowashukia walikunja mikono yao wakaondoka. Na halafu, wanawake siku hizi katika kanisa la Kipentekoste wakikata nguo zao, na kutenda. . . halafu bado unasema una Roho Mtakatifu. Kuna baadhi. . . Mimi—mimi ni. . . Nawapenda, mnajua hivyo, lakini mimi—mimi—mimi nina

bidii. Ninapomwona dada yangu, binti wa Mungu, huko nje, nimwone ndugu yangu mwoga kiasi cha kulazimika kusimama nyuma ya aina fulani. . . anashindwa kuhubiri Neno la Mungu, kwamba anajua ukweli, nimwone dada yangu akijiendesha kama mwanamke fulani wa mitaani badala ya mtakatifu wa Mungu, nimwone mtu fulani anayeogopa kusimama na kutangaza ukweli, akiogopa dhehebu lake litamfukuza, mwana wa Mungu, sininii. . . damu hiyo haitoki vizuri. Ukristo halisi wa kweli huliamini Neno, na kulishikilia, huishikilia ahadi hiyo.

199 Sasa, ninyi ni wageni. Mimi, nikitazama huku na huku, namjua Ndugu Williams aliyeketi hapa. Ninamwona Dada Moore, nafikiri huyo ni Dada Boutliere anayeketi karibu naye, sikumtambua jana usiku. Ninajaribu kuona kama ninamwona mtu yeyote ninayemjua. Ndugu huyu hapa, si—siwezi kulikumbuka jina lake. Yeye. . . [Mtu fulani anasema, "Ndugu Harris."—Mh.] (Ati nini?) ["Ndugu Harris."] Ndugu Harris, ninamjua. Ndugu na Dada Dauch, wanaoketi papa hapa, kutoka Toledo, huko Ohio. Karibu ni hao tu, ni, ninaamini ninamwona Ndugu Collins. Hiyo ni kweli, Ndugu Collins? Maskini mvulana mzuri wa Methodisti, aliyempokea Roho Mtakatifu, ni mmoja wa mashemasi wangu kanisani sasa. Mungu akubariki, Ndugu Collins, Dada Collins.

200 Roho Mtakatifu anaingia sasa. Inakuwa kupofushwa, laiti ningaliweza kuelezea hili. Huwezi kumwelezea Mungu, huna budi kumwamini Mungu, uwe tu na imani, usiwe na shaka, mwamini Bwana Yesu Kristo. Biblia inasema unapaswa kuokolewa ikiwa unaamini.

201 Unasema, "Bwana, mimi ni kama yule mwanamke aliyegusa mavazi ya Bwana, sijaribu kumgusa mhubiri huyo, yeye ni mwanadamu, lakini Biblia ilisema kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu ambaye anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Je, alisema hivyo? Hilo ni Agano Jipya. Vema, basi ukimgusa Kuhani Mkuu, ungejuaje kuwa ulikuwa umemgusa isipokuwa Yeye atende sawasawa na alivyotenda jana? Na ikiwa Yeye ni yeye yule, atafanya vivyo hivyo. Je, hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli? Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Basi ilikuwaje wakati mwanamke huyo alipomgusa kisha akaenda zake na kuketi kama mnavyoketi, ama chochote alichofanya? Yesu aligeuka na kusema, "Mtu alinigusa."

Petro akasema, "Mbona, kundi zima limekugusa Wewe. Kwa nini kusema jambo kama hilo?"

202 Akasema, "Lakini naona kwamba nguvu, ni. . . zilinitoka, nikadhoofika." Akatazama huku na huku mpaka akampata yule mwanamke, akamwambia juu ya kutokwa kwake na damu, na kusema, "Imani yako imekuokoa."

203 Yeye ni Mungu yeye yule usiku wa leo, Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, sasa aminini. Aminini, ninyi ambao hamnijui,

ninyi ambao hamna kadi za maombi, mwombeni Mungu, na muwe wanyenyekevu kuhusu jambo hilo. Sasa, kumbukeni, itahitaji imani yako kumgusa, siwezi kumgusa kwa niaba yako, huna budi kumgusa wewe mwenyewe, ni imani yako mwenyewe, lakini wewe amini. Ni wangapi wanaoamini? Semeni, "Naamini." " . . . unaweza kuamini . . . " Hebu tuanze tu, safu kwa safu, amekuja hivi punde.

204 Sasa, laiti mngalininii kabisa . . . Msiamke na kuzunguka sasa, kaeni kimya kabisa. Bwana Mungu na alijalie Kanisa Lake uthibitisho. Mungu, nimesema ukweli, kadiri nijuavyo ni kweli. Baba wa Mbinguni ambaye tutasimama mbele zake, na ajalie hili litendeke kuwasaidia watu Wako, Bwana, kuwasaidia watu Wako. Kuhubiri kwa nguvu, huna budi kuninii . . . ni badiliko, ni upako mwingine; ni Roho yeye yule, ila tu ofisi nyingine.

205 Mama anayeketi hapo, papa hapa mwishoni mwa safu, papa hapa akiniangalia, hicho kitu kidogo cheupe juu yako, unaamini? Unaamini? Unaniamini mimi kuwa mtumishi Wake? Una haja Naye, sivyo? Ni kwa ajili ya koo lako. Muulizeni kama hiyo ni kweli. Bibi Sparks, unaamini kwa moyo wako wote? Mtoto huyo anayeketi hapo, unataka aombewe pia. Naam, bwana. Ana upungufu wa damu, ana ugonjwa wa fadhaa; hiyo ni kweli, sivyo? Simjui huyo mwanamke, sijawahi kumwona maishani mwangu. Weka mkono wako juu ya huyo mtoto.

Katika Jina la Yesu Kristo, kama mwanamke huyu alikuwa na imani ya kutosha kufanya hivyo, na ijulikane, Bwana, jalia uondoke katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Usitie shaka. Sasa, Yeye yuko hapa. Unaona? Tulikuwa tukimsifu mpaka aje, sasa Yeye yuko hapa.

206 Huyu hapa maskini mwanamke ameketi hapo nyuma, nyuma ya mwanamke huyo. Ameinua mikono yake juu, anayo leso mkononi mwake, anaomba, ameketi mwishoni. Huyo mwanamke anasumbuliwa na tumbo, imekwisha, dada. Je, una kadi ya maombi? Huna? Huihitaji. Huna, nenda nyumbani ukale chakula chako cha jioni, imekwisha kabisa.

207 "Kama unaweza kuamini . . . " Je, unaamini? Waulizeni watu hawa, Mungu Mbinguni anajua sijawahi kuwaona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Ikiwa si Kristo yeye yule . . .

208 Hapa, huyu hapa maskini mwanamke aliyeketi papa hapa, amevaa koti jekundu. Je, una kadi ya maombi, mama? Huna? Huhitaji moja. Wewe sio mgonjwa, bali una swali niani mwako ambalo unataka kunizungumzia kulihusu, na swali hilo ni tatizo la kiroho: Unataka kujua kama unataka kuacha kazi yako na kuingia katika kazi ya wakati wote kwa ajili ya Bwana. Wewe si wa hapa, unatoka Texas, Houston. Vumilia, atakuita atakapokuwa tayari kwa ajili yako. Sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Ninakusahi kuamini.

209 Ati nini? Huko nyuma kabisa. Hapa, haya hapa mawasiliano mazuri ya mtu na Roho, mwanamume aliyeketi papa hapa nyuma, shati jeupe, kidogo ana upara, anatoka Arkansas. Je, una kadi ya maombi? Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Shida yako ya tumbo imekuacha, unaweza kurudi nyumbani Arkansas ukishangilia. Sijawahi kumwona maishani mwangu.

210 Huyu hapa mtu ameketi hapa aliye na pumu, ngiri, ametoka Texas, Bw. Cobb, hiyo ni kweli, hatufahamiani. Unaamini? Rudi Texas ukawe mzima, katika Jina la Yesu Kristo. Yeye ni Mungu. Unaamini?

211 Hapa, huyu hapa msichana mdogo, mnene ameketi hapa. Una kadi ya maombi, kipenzi? Je, unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu? Kama mtumishi wa Mungu, unaamini nilichokisema muda mfupi uliopita katika ujumbe huo ni kweli? Shida yako ya figo itakuacha, nenda nyumbani, ukapone katika Jina la Yesu Kristo.

Amini.

212 Mwanamke aliyeketi papa hapa, mwishoni mwa safu, aliye na maambukizi ya sikio. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Nenda nyumbani, amini, uwe mzima.

213 Kuna mwanamke aliyeketi pale aliye na ugonjwa wa moyo, amevaa kofia ya zambarau, jina lake ni Bibi Lambert. Je, unaamini kwa moyo wako wote? Shida yako ya moyo itaondoka, unaweza kwenda nyumbani na kuwa mzima.

214 Unaamini? Unaamini? Ninakusahi uamini. Inua mikono yako.

215 Bwana Yesu, Mwana wa Mungu, jalia mambo haya yasipite, Bwana, hutendi mambo haya bure. Wewe ni Mungu, Mungu wa Milele, unaishi milele. Na ijulikane usiku wa leo ya kwamba Wewe ndiwe Mwandishi wa hili, maagizo ni sahihi. Wewe uko miongoni mwetu, na Wewe ni Mungu. Jalia watu wakuamini Wewe sasa, na jalia wapate kuponywa, tiba maradufu kwa kutokuamini kwote, na mambo yote. Tunakupa sifa, Mungu wetu mwenye neema, Baba yetu wa Mbinguni. Katika Jina la Yesu Kristo, tunawakabidhi Kwako.

216 Je, unaamini, kwa moyo wako wote? Zungumza na baadhi ya watu hawa, sijawahi kuwaona maishani mwangu. Sijui wana shida gani sasa, Huyo ni Roho Mtakatifu, hilo ni thibitisho kwamba nimewaambia kweli: Njia ya kurudi ni vile nilivyowaambia. Kanisa limepotea nyikani, likitangatanga. Mungu, Baba yetu, yuko hapa miongoni mwetu ndani yetu, kama alivyokuwa ndani ya Mwanawe, Kristo Yesu, ila tu alikuwa ndani Yake bila kipimo, ndani yetu kwa kipimo, bali Roho yeye yule. Hivi hamwezi kuliona? Je, hamjui hilo? Amini kwa moyo wako wote.

217 Tuko wapi? Mwaminini Mungu, aminini mambo haya ambayo Yesu alisema. Angewezaje kuwa Mwana wa Mungu na aseme uwongo? Anawezaje kutoa ahadi, wala si ya kweli? Ni kwa sababu hatujachanjwa, hatujarudi kwenye ile Zeri, hatujarudi na kumwacha Roho Mtakatifu halisi, sio mhemuko, si msisimko, hata hivyo ni msisimko, hata hivyo ni mhemuko, bali mwacheni aingie na kujithibitisha Mwenyewe. Jiwekeni wazi, atafanya mambo ambayo alifanya daima, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Je, mnaamini Hilo sasa?

218 Ni wangapi walio na kadi za maombi sasa? Inueni mikono yenu. Ikiwa mnaniamini mimi kuwa mtumishi wa Kristo . . . Yesu alisema, agizo la mwisho kwa Kanisa, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya." Ninajisikia kuongozwa, nilitaka kutoka nje, lakini kitu Fulani kikaniambia, "Usifanye hivyo, hao watu wanataka uwawekee mikono." Mungu ni mwema, alinikatiza kutoka kwa mawazo yangu mwenyewe. Ni nini kilicholizuia? Ulifanya hivyo, kwa shauku yako; atakupa shauku ya moyo wako. Pangeni mstari, ninyi mlio na kadi za maombi, njoni moja kwa moja upande huu na mpange mstari. Yeye ni mwema.

219 Nilimwona akiishusha ndege kutoka angani, akanishikilia pale usiku kucha, na siku nzima kesho yake ili . . . kwa ajili ya imani ya mwanamke mweusi kwa ajili ya mvulana wake anayekufa. Hakika. Mnaamini? Je, mnauamini Ujumbe? Kama hamwezi kuuamini Ujumbe, vema, kamwe hamtamwamini mjumbe, nina hakika. Lakini kama ni Ujumbe, Mungu atauthibitisha.

220 Sasa, mnaona kile maono yafanyacho. Mimi . . . Maono ni kitu kinachotoka kwa Mungu, maono hayakuponyi, maono yanamtangaza Mungu. Biblia ilisema, "Akiwako mtu miongoni mwenu, anayedai kuwa nabii, Mimi Bwana nitasema naye." Angezungumzaje? Kama alivyofanya, alivyonena sikuzote. "Na vipi kama akisema, ukweli, nitathibitisha kwamba ni kweli." Basi chukueni hayo maagizo na mrudi, mwirudie imani ya Kipentekoste. Uwe ndugu, Umoja kwa Utatu, Utatu kwa Umoja. Uwe ndugu, Church of God kwa Mnazarayo, Mnazarayo kwa Church of God. Kuwa ndugu, kuwa dada, msiruhusu madhehebu yawatenganishe. Mungu alilichagua Kanisa Lake tangu zamani, wako kwenye kidimbwi mahali fulani, inatupasa kutoka tukawalete. Roho Mtakatifu yuko hapa usiku wa leo akichunguza kila moyo, Mungu wa Mbinguni na awajalie . . .

221 Sasa, wakati ninyi watu mnapokuja, kama ningeweza kuwaponya, ningefanya hivyo, lakini kama ningewaambia ningeweza kuwaponya, ningesema uwongo, tayari mmeponywa, Yesu aliwaponya alipokufa pale Kalvari, kwa maana "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tulipona." Ni wangapi wanaoamini hiyo ni kweli? Semeni, "Amina." Kitu pekee ninachoweza kufanya ni kuwawekea

mikono na kuwatakia baraka, Mungu, jalia baraka hii, hiyo itawasaidia, nina hakika, kama mtaamini, kama Oral Roberts alivyosema wakati mmoja, ni kituo cha mawasiliano.

222 Ninataka kila mtu hapa ndani aamini sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu na kuomba. Ninataka watu hawa wapange mstari papa hapa, na wanapopita, nitaomba sasa, niwawekee mikono. Inachelewa, inaelekea saa nne, nami nitawaombea. Nitawaombea sasa hivi, nitawawekea mikono.

223 Nitawaomba ndugu wahudumu, ili kwamba mwone sio mimi tu, sio mimi pekee, mhudumu yeyote ana haki ya kuwaombea wagonjwa. Mhudumu yeyote ambaye ni mtauwa na ametumwa na Mungu, ambaye anamwamini Mungu, Mungu atasikia maombi yake vile vile atakavyomsikia mtu yeyote, huenda wasiweze kupambanua na kadhalika namna hiyo, hawawezi, hilo halitukii mara nyingi sana. Hiyo ni kweli. Lakini hiyo haimfanyi mtu anayefanya hivyo zaidi ya mtu mwingine yeyote.

224 Siwezi kuhubiri kama wahubiri wafanyavyo, siwezi kufundisha kama mwalimu afanyavyo, siwezi kunena kwa lugha kama karama ya lugha, sina tafsiri. Imenijia, loo, mara moja au mbili, nimenena kwa lugha mara nne au tano maishani mwangu. Lakini sikuwahi kuninii...Ha—ha—hakika nilihisi hivyo mara nyingi, lakini haikutamkika. Ilifanya hivyo mara kadhaa. Nilifanya hivyo wakati mmoja...Nilinena kwa lugha kwa muda wa saa moja wakati mmoja. Nilikuwa nikinena kwa lugha wakati mmoja, hata sikujua nilikuwa nikifanya hivyo. Nikaangalia pande zote nione ni nani aliyekuwa anaongea, nikawaza, “Yuko wapi huyo Mjerumani, yeyote yule?” Kuangalia pande zote, ilikuwa ni mimi nikizungumza, nilitulia tu kabisa. Wakati uo huo kulikuwa na mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu karibu maili kumi kutoka pale, akijaribu kufika kanisani, ndipo alipofika pale, akatoa ushuhuda, aliponywa papo hapo, ilikuwa ni Roho Mtakatifu akifanya maombezi. Hakika.

225 Sasa, mambo hayo si ya uongo, marafiki, ni kweli. Mungu Mbinguni anajua ni kweli, maelfu ya mambo kama hayo, makumi ya maelfu. Kwa hiyo, ni Mungu, marafiki, ni Mungu. Amini kwa moyo wako wote sasa.

226 Ndugu Moore, baadhi yenu ndugu, Ndugu Tracy, yeyote wenu ndugu wahudumu, anayetaka kusimama pamoja nami hapa, ninapowekea mikono. Ndugu Don, ungeweza kuwasaidia pale, Ndugu Brown, mtu yeyote, yeyote wenu ninyi ndugu ambao ni Wakristo, na mnaaminini, njoni hapa mkaombe. Hebu sote tuinamishe vichwa vyetu sasa.

227 Mungu wa neema, tuko hapa kusaidia. Ninaomba ya kwamba Wewe utasaidia, Bwana, wanajua Wewe uko hapa. Wanajua kwa tunda la Roho, wanaona kwa matendo ya Roho Mtakatifu kwamba Wewe uko hapa. Bwana, sisi ni wanadamu tu, tumesimama hapa kushughulikia ofisi yetu, “Ishara hizi

zitafuatana na hao waaminio, wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Bwana, na iwe kwamba kila mtu apitaye atapona, tunapoweka mikono yetu juu yao katika kumbukumbu ya huruma yetu kwao, na imani yetu kwa Mungu.

228 Kwanza kabisa, ninaweka mikono yangu juu ya mtoto huyu, na kulaani kichwa hiki kilichojawa maji, na, katika Jina la Yesu Kristo, na kipungue, jalia huyu mwanamke arudi, akionyesha kichwa cha mtoto huyu kilipunguka kiasi gani, jalia aishi kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Amina.

Mkono wangu juu ya ndugu, katika Jina la Yesu Kristo, na apone.

Mkono wangu juu ya ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo, na apokee uponyaji wake.

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yangu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, huyu mtoto na aponywe.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia dada yetu aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, naomba dada yetu aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia ndugu yetu aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia ndugu yetu awe mzima.

Wakristo wote wanaomba sasa, kila mtu anaomba.

Katika Jina la Yesu, jalia nanii wetu...?...

Wawekeeni mikono, ndugu.

Katika Jina la Yesu Kristo naomba dada yetu...?...

229 June, usiamini unachowazia, utakuwa mzima, June. Mama, haya yalikupata, lakini nilipoambiwa jana usiku, leo nilikuwa katika maombi. Unapitia kwenye kitu kama kuzingirwa kama Bibi Moore, ama kitu kama hicho, lakini utakuwa mzima...?... Mungu wa Mbinguni na aziweke baraka Zake juu ya msichana huyu...?...Katika Jina la Yesu Kristo, kila mshipa na uachilie, na arudi mara moja hadi mahali ambapo sauti hii ya kupendeza sana, talanta hii ambayo imetolewa kwa Ufalme wa Mungu, naomba tuisikie ikirudisha mwangwi kote nchini tena. Ninamkemea ibilisi ambaye anajaribu kuyapofusha macho yake, na kujaribu kutia sumu akilini mwake kwa mambo haya, lakini jalia Mungu wa Mbinguni apite kwa mwangaza wa mchana wa Nuru ya Kristo. Ninadai msichana huyu kwa ajili Yako. Ulisema, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usiwe na shaka moyoni mwako, lakini uamini ya kwamba uliyosema, yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako." Ninamtatangaza msichana huyu kuponywa, katika Jina la Yesu Kristo. Yamesemwa, sasa na yatimie.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia hili lifanyike kwa ajili ya ndugu yetu.

230 Dada Schrader, nilipata barua yako, namjua Dada Schrader, uliniuliza kuhusu ile kanda, sijawa nyumbani bado kuisikiliza, nitaipata nikifika nyumbani.

231 Dada Schrader, wewe ni mwanamke mzuri, nakupenda, dada yangu. Wewe ndiye, mimi pasipo kukujua, nilipoingia na mtu fulani akanena kwa lugha, nawe ukatoa tafsiri, na kusema jambo lile lile ambalo Nuru ile ilisema, iliposhuka juu yangu kule chini, mara ya kwanza nilipokuwa maskini mhubiri wa Kibaptisti. Kasema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia Kuja Mara ya Kwanza kwa Kristo, umetumwa, na Ujumbe wako utakutangulia Kuja Mara ya Pili."

Wakati yule mhudumu wa Kibaptisti, ambako niliwekwa wakfu, aliposikia jambo hilo, kasema, "Ati mtu mwenye elimu ya darasa la saba atawahubiria watawala?"

Nikasema, "Hivyo ndivyo Yeye alivyosema."

232 Gazeti likasema, *Nuru ya Ajabu Inaning'inia Juu ya Mhudumu*, ilikuwa kwenye Associated Press. Bila kujua lolote kuhusu hilo, miaka kumi na mmoja baadaye, mtu mmoja akanena kwa lugha, nawe ukafasiri jambo lile lile, nami nilikuwa nimesimama pale. Mungu yuko pamoja nawe, Dada Schrader, ibilisi anakuonea, mimi ni ndugu yako. Ee Bwana, Muumba wa Mbingu na nchi, maskini mwanamke huyu dhaifu, ambaye mpendwa wake wa thamani ametuacha, Ee Bwana, jalia zile Nguvu zilizomfufua Mwokozi wetu kutoka kaburini, jalia aje juu ya maskini umbo hili dhaifu kwa utukufu Wako, ambaye anatabiri katika Jina Lako, na ajitokeze. Pia jalia karama hii ambayo imebanwa, na irudi vyema, jalia apone, Bwana; ninautangaza juu yake, katika Jina la Yesu Kristo. Sasa, imesemwa, Bwana, na itendeke kwa utukufu Wako. Mungu akubariki, dada. Nafsi yako . . .?. . .

Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo mbariki dada huyu mchanga na umpe kile anachoomba, katika Jina la Yesu.

Mungu ambariki ndugu yetu, na ampe uponyaji wake katika Jina la Yesu Kristo.

Mungu ambariki dada yetu, ampe uponyaji wake, katika Jina la Yesu Kristo.

Mungu ambariki ndugu yetu, mpe, Bwana, uponyaji wake.

233 Jalia watu wanaopitia hapa, watambue Bwana, sio kupita tu kwa urahisi, bali waje kwa imani, wakiamini, hiyo ndiyo njia ya kuupokea, ikiwa wengine . . .?. . . Tujalie, Bwana. Jalia wasije, wapitie tu hapa kwa uchaji, bali na watambue wanakuja chini ya baraka za Mungu, ambazo zimethibitishwa usiku wa leo kanisani, na ya kwamba Yeye yuko hapa, huku Neno Lake limethibitishwa na kuhakikishwa. Bwana, hakuna nguvu za uponyaji ndani yetu, tunaweza kuifanya hivyo, tunafuata tu

lile agizo, kama vile tulivyoagizwa kwenda kuwabatiza watu, Yeye aliahidi kuleta Roho Mtakatifu, hilo ndilo tu tunaloweza kufanya ni kubatiza, kuhubiri Neno na kubatiza. Ndipo ninaweza kuhubiri Neno, Wewe ulithibitishe, nami ninaweka mikono juu ya watu hawa. Mungu, wafanye. . .?. . .katika Jina la Yesu. . .?. . .

Mungu, vivyo hivyo kwa ndugu huyu, mpe baraka zizo hizo, katika Jina la Yesu.

Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu mponye dada yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo mponye huyu dada yetu, jalia uishe tangu usiku wa leo na kuendelea.

Bwana, Kanisa Lako kuu hapa linaomba, Baba. Na iwe kwamba watu hawa waponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia uponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye ndugu yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo, na litendeke kwa ajili ya nanii wetu. . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, na litendeke. . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, na litendeke kwa ajili ya dada yetu.

234 Katika Jina la Yesu Kristo, mpe dada yetu imani hii ya ushindi sasa hivi, kwamba yuko Mbele za Mwana wa Mungu, Yule anayeenea kila mahali papa hapa sasa. Na akujalie ninii yako. . .?. . .

Vivyo hivyo kwa ndugu yetu, na aamini, anapopita.

235 Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Ulisema wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya, ninakuamini, Bwana, na katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya wagonjwa hawa.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu. Baba yako, na aongeze juu ya baraka ambazo amekuwa nazo. . .?. . .

Mungu ajalie katika Jina la Yesu uponyaji wa dada yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia uponyaji wa ndugu huyu.

Mungu, jalia shauku ya ndugu yetu, tunaomba, katika Jina la Yesu.

Baba wa Mbinguni, jalia shauku ya dada yetu katika Jina la Yesu Kristo.

Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, mjalie dada yetu. . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia uponyaji wa dada yetu.

Katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, mjalie uponyaji wake, Baba.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye ndugu yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo, Bwana, mponye ndugu yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia uponyaji wa ndugu yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia uponyaji wa ndugu yetu.

Mponye dada yetu, Baba Mungu.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yetu, Baba.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yetu.

Katika Jina la Yesu, mponye ndugu yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yetu.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye ndugu yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada huyu na mtoto huyu mchanga kwa ajili ya utukufu Wako.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu, dada yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo, Bwana, mponye huyu, dada yetu, ninaomba.

Katika Jina la Yesu Kristo, baraka za Mungu zimwendee . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye ndugu yetu.

236 Unapopitia, amini—amini. Je, Yeye anawezaje kufanya mambo haya anayofanya kama hayupo hapa? Yeye ni mkuu tu . . . upako ule ule tu hapa kama wakati wowote.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu, dada yetu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya dada yetu, Bwana.

Katika Jina la Yesu Kristo, amini hilo. Amina. Amini hilo sasa . . .?. . . dada. Mungu akubariki.

Katika Jina la Yesu Kristo huku mikono yangu . . .?. . . katika Jina la Yesu.

Katika Jina la Yesu Kristo . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo . . .?. . .

Katika Jina la Yesu ndugu yetu na aponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia dada yetu aponywe.

Mponye dada yetu, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo.

Katika Jina la Bwana Yesu, mponye huyu, dada yetu.

Mponye dada yetu katika Jina la Yesu Kristo.

Baba, katika Jina la Yesu, mponye dada yetu, ninaomba.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye ndugu yetu . . .?. . .

237 Hii . . . (Je, utakata swichi hapo?) Hili hapa linaweza kuonekana la kigeni sana, lakini ni kutii tu tendo la Mungu. Ikiwa unaamini kwamba ulitubu, umebatizwa, wewe ni mtaradhia wa Roho Mtakatifu. Unaona? Kwa nini? Kwa mhudumu, mtumishi wa Kristo, ambaye amewaletea ile Kweli, kuwahudumia Neno la Mungu, basi kama Mungu akija katika Neno Lake nao wanahubiri Neno, naye Roho Mtakatifu anashuka na kuthibitisha Hilo kuwa ni kweli.

238 Mnaona, marafiki, kile kilichotukia muda mfupi tu uliopita, si—sijui mimi, Mungu Mbinguni anajua sijui. Mnaona? Lakini chochote kilichokuwa, lazima kilikuwa cha utukufu kwa sababu moyo wangu unadunda kwa kasi sana kwa furaha, kilikuwa ni kitu kwelikweli.

239 Sasa, inaonekana kwangu kama, kwamba kanisa lililozaliwa mara ya pili linalodai kuzaliwa upya, na ni . . . wakati wa Kuja kwa Kristo umekaribia . . . Mbona, pamoja na ushahidi, ushahidi chanya . . .?

240 Kama kungekuwa na mtu amesimama hapa amevaa joho refu, na makovu mkononi mwake, damu ikitoka usoni mwake, huyo bado asingekuwa ni Kristo, mdanganyifu yeyote angeweza kufanya hivyo; bali Maisha yaliyokuwa ndani ya Kristo yakiletwa tena, basi unajua ni Kristo.

241 Ninahubiri moja ya siku hizi usiku juu ya: *Kitendawili*, na hicho mlichokiona hivi punde kilikuwa ni kitendawili, ni jambo ambalo haliwezi kuelezeka. Mnaona? Ni mwujiza, jinsi Mungu wa Mbinguni anavyoweza kufanya hivyo. Sasa, unasema, "Ungeweza kuniponya, Ndugu Branham?" Haiwezekani, tayari umepona.

242 Kama angalikuwa amesimama hapa, amevaa suti yangu aliyonipa, asingeweza kufanya cha zaidi, hilo tu ndilo angeweza kufanya ni kuthibitisha kwamba Yeye ni Kristo, kuthibitisha ya kwamba Yeye yuko hapa, huna budi kumwamini, "Ninaweza, ikiwa unaamini." Hilo ndilo sasa hivi, ikiwa unaamini, hakuna lingine. Inaonekana kwangu kama inapaswa kushitusha sana, inapaswa kuwapeleka watu wakatubu, inapaswa kuwapeleka watu kumtafuta Roho Mtakatifu, inapaswa kufanya jambo fulani zaidi ya inavyofanya.

243 Hivi Wa- . . . hivi—hivi Neno Mbegu linaanguka sehemu yenye mawe? Enyi kina mama, jibu ni lipi? Enyi ndugu, kanisa, jibu ni lipi? Mungu anaweza kufanya nini cha zaidi? Kamwe hakuahidi jambo lingine, hutaona jambo lolote kubwa kuliko Uwepo wa Yesu Kristo ukifanya kazi katika Kanisa Lake, ukifanya mambo ambayo Yeye aliahidi kufanya.

244 Lakini unajua, kuna jambo lililotendeka kwa Kanisa. Je, mnadhani ingekuwaje kama miaka hamsini iliyopita *hilo* lingalitokea? Mnaona, haina budi kuwa na nguvu zaidi sasa kulitikisa Kanisa kwa nguvu zaidi. "Adui anapoingia kama mafuriko, Roho wa Mungu huinua kiwango dhidi yake." Moja ya siku hizi ataliinua Kanisa moja kwa moja kutoka mahali Pake, wale watakatifu waliozaliwa mara ya pili. "Wawili kitandani, nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja; wawili kondeni nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja." Italiinua Kanisa hadi kwenye Uwepo wa Kristo lipate kuishi milele. Sisemi hivi ili kuwa fidhuli, nasema kwa upendo wa kiungu, udugu, unyofu, nikiwa na nja—njaa moyoni mwangu kuona Kanisa la Mungu likiwa Kanisa la Mungu, mwili wa watu.

245 Wanadamu hawawezi kukufanyia lolote, unapopitia kwenye mstari huu namna hiyo, ukiwekewa mikono. Mmesikia vitimbi vingi sana, na mengi sana, [Ndugu Branham ananusa-nusa—Mh.] "Nanusa . . . " na aina hii yote ya mambo ambayo hata si ya Kimaandiko, karibu yameziduwaza akili zenu. Mnaona, ibilisi alifanya hivyo ili kuwatikisa mtoke kwenye ile Kweli, Neno ndilo Kweli, na Neno limefanyika mwili. Mnaelewa? Mungu awabariki nyote. Nawapenda. Hapa kuna leso. [Dada mmoja anatoa ushuhuda—Mh.] Amina. Mungu asifiwe.

246 Bwana Yesu, Ua la Uwandani, Ninyoro ya Bondeni, Nyota ya Asubuhi, Shina na Mzao wa Daudi, Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho, Yeye Aliyekuwako, Aliyeko, na atakayekuja, tuma baraka Zako, Bwana, juu ya watu hawa. Wabariki, Bwana, kwa uamsho wa mtindo wa kale, uwarudishe, Bwana, kwenye ujuzi ambao baba na mama zao walikuwa nao miaka mingi iliyopita, ambao tunausherehekea, katika mkutano huu.

247 Hizi hapa leso. Walizitoa kutoka katika mwili wa wale watakatifu wa kale waliobarikiwa miaka hamsini iliyopita, wagonjwa wakaponywa, miaka elfu mbili iliyopita walifanya jambo lile lile, nao waliponywa. Wewe ni Mungu yeye yule usiku wa leo, Roho Mtakatifu yeye yule, akija kwa wingi sana, na nguvu zikirejeshwa kwa Kanisa, kulitikisa Kanisa litoke katika usingizi Wake. Kila atakayevaa leso hizi na aponywe, Bwana, nguvu za Mungu na zimfanye kila mmoja awe mzima, ninazituma katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya uponyaji.

248 Wabariki watu sasa, ninawakabidhi Kwako, Bwana. Neno limehubiriwa. Umejidhihirisha Mwenyewe, umethibitisha ya kuwa Wewe uko hapa, umethibitishwa ya kuwa hujafa, bali umefufuka katika wafu, na U hai hata milele, yeye yule jana, leo, na hata milele, ukitimiza amri Zako, na kulitimiza Neno Lako na ahadi Zako kutoka kizazi hadi kizazi kwa yeyote atakayeliamini Jina Lako.

249 Roho Mtakatifu mkuu, akitafuta ampate mtu mahali fulani. Ee Mungu, Yeye alimpata Ireneo fulani siku moja, alimpata

Polikapu fulani siku moja, alimpata Paulo fulani siku moja, alimpata Martin fulani siku moja, alimpata Luther fulani siku moja, alimpata Wesley fulani, alimpata George Whitefield fulani, Ee Mungu, alimpata Billy Sunday fulani. Mungu, jalia atupate usiku wa leo, Ee Mungu, mtu wa majira haya anayeweza kulitikisa Kanisa kwa njia kama hiyo kwa kuihubiri Injili, kama Charles Finney fulani, ama mtu fulani, Bwana, ambaye atalirudisha Kanisa mahali Pake tena. Wakati Roho Mtakatifu mkuu Mwenyewe, kazi yake Mwenyewe, sio mwanadamu, atakapoingia miongoni mwa watu, na kujitangaza Mwenyewe kama alivyofanya usiku wa leo, tunakushukuru Wewe, Bwana.

Pokea shukrani zetu, na utupe baraka Zako. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza

250 Hebu na tufumbe tu macho yetu sasa, na tuinue mikono yetu, na tumpe Yeye sifa. Mnajua Yeye yuko hapa. Ni wangapi wanaoamini hilo kwa moyo wenu wote, kila kitu, wanaamini ya kwamba Kristo yuko hapa? Semeni, "Amina."

Sasa, hebu tumwimbie Yeye sasa, kwa moyo wetu wote ulio ndani yetu, na kumpa sifa zote tujuavyo kumpa. Sasa, vema.

Na . . .

Fungeni tu macho yenu sasa, katika Roho, tuimbe.

. . . penda . . .
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

251 Loo, ajabu. [Ndugu mmoja ananena kwa lugha na kufasiri—Mh.] Amina. Je, mnajua hiyo ni nini? Ni nini? Kunena kwa lugha na kutafsiri ni nini? Kudundadunda kwa Roho Mtakatifu akizungumzia jambo ambapo hujui unachosema. Unaona?

252 Nimewaambia njia ya kurudi, ninawapa mwaliko: Je, ni wangapi hapa wangependa kuchukua njia hiyo na kufuata maagizo? Wengi wenu hapa ambao hamjapata kubatizwa, na mngependa kubatizwa, inua mkono wako, useme, "Ninaamini, niko tayari, nitafanya kazi zangu za kwanza, nitarudi tena, nitamjia Kristo." Inua mkono wako. Kutakuwa na ibada ya ubatizo hapa kesho usiku.

253 Mhudumu wa Kibaptisti ametuma neno hivi punde tu, akasema, "Niko tayari." Vema. Ndugu, mimi natoka kanisani mwako pia, walinisomea yale maagizo vibaya, lakini niliyasoma mwenyewe, niligundua baada ya kubadilisha, na kuyasoma, na kufanya jinsi Yeye alivyosema yafanywe, jambo fulani lilinipata. Ee Mungu, tuma Nuru. Mwangalie Yeye akiita. Nashangaa ni kwa nini sisi—kwa nini tunafanya hivyo?

254 Ni—ninathamini uvumilivu wenu, jinsi tunavyoketi na kungojeana, kwa sababu ni Roho Mtakatifu akijaribu kuingiza kitu ndani yetu, mnaona, Yeye anajaribu kuingiza kitu fulani. Uvumilivu wenu ni mzuri sana, na hilo linafaa. Ukisema, "Loo, sielewi, lakini nitaketi na kuliona, sina budi kulitazama," Mungu atajaza kila moyo wenye njaa ambao—ambao kweli utajitolea. Unapoliona, usingojee dakika nyingine, nyosha mkono ulichukue, papo hapo, linapita, huenda asipite njia hiyo tena. Hiyo ni kweli.

Amina! Amina!

255 Shh, shh, tu! [Dada mmoja ananena kwa lugha naye ndugu mmoja anafasiri—Mh.]...?...Amina. Ashukuriwe Bwana. Je, mliona? Alisema alikuwa hapa kupokea sifa zetu. Mnajua lile pambio la *Amina*, ambalo Ndugu Zepp huimba, ambalo yeye...? *Amina*? Nyinyi huliimba, sivyo? Vema, Ndugu Don. Vema. Huh?

256 Hima, Ernie. Tutampa sifa kwa ule wimbo wa *Amina*. Wewe...Ni wangapi wanaoujua? Loo, sote tunaujua, naamini. Kanisa langu lote linaujua, ninaamini, ama ni—nilidhani labda wewe...Wasemaje? Loo, ndugu, nisingeweza kuuongoza, si—siwezi kuimba. Loo, lakini nadhani hilo litakuwa jema sasa hivi, kusema, "Amina!" kwa kila kitu alichosema. Loo, jamani!

Amina! Amina! Amina! Amina! Amina!

Amina! Amina! Amina! Amina!

Kila mtu, uimbeni.

Amina! Amina! Amina! Amina! Amina!

Amina! Amina! Amina! Amina! Amina!

Amina! Amina! Amina! Amina! Amina!

Amina! Amina! Amina! Amina! Amina!

257 Hebu tuinue mikono yetu na kumpa Yeye...?... Tunakusifu Wewe, Bwana, kuniokoa na kunibariki. Mtume Roho Mtakatifu, Bwana. Njoo usiku huu na...?...kila moyo huku tukisifu...?...

62-1123 Njia Ya Kurudi
Life Tabernacle
Shreveport, Louisiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org